CHUO CHA BIBILIA

Mwanzo - Kutoka

KITABU CHA # 1

Utangulizi

Karibu katika Chuo cha Bibilia. Tutakua tukijifunza Bibilia kutoka mwanzo hadi mwisho pamoja katika mfululizo wa mafunzo uliomo kwenye vijitabu 30. Safari yetu ya ufahamu itatuchukua kutoka kitabu cha Mwanzo hadi Ufunuo. Tutatizama kila kitabu kwa kupitia juu juu kila kitabu ambacho kipo katika Bibilia, na kutizama ramani yake, kisha tutakitizama kwa undani zaidi ili tuweze kuyatenda yale tuliyojifunza.

Bibilia ni kitabu ambacho cha weza kukutia bumbuazi. Ni vigumu kufuatilia yale yaliyo tendeka, mahali yalipotendeka, ni nani inayehusishwa na maana ya yale yote yanayotokea. Lakini kila kifungu cha maandiko na kila chembe ya fumbo ni sehemu tukufu ya bibilia nzima kwa ujumla. Tufikapo mwisho wa safari yetu pamoja, maombi yangu ni kwamba utakuwa umepokea ufahamu zaidi ya jinsi Bibilia inavyo shikamana pamoja. Baada ya kuvipitia vitabu vyote vya Bibilia, utakuwa umepokea picha bora ya kila kimoja na utaweza kuviweka katika sehemu inayotakikana katika hadithi yake Mungu. Utakuwa umetambua jinsi Mungu alivyoitenda kazi katika nyakati za Agano la Kale, na utakuwa umejifunza yale yaliyo badilika baada ya kuja kwake Kristo na ni kwa sababu gani. Yale ambayo umeyaamini katika moyo wako yatathibitishwa katika nia yako, pia utakuwa na ujuzi mpya katika ujasiri na ufahamu wako katika kuieleza imani yako kwao watu wengine.

Ni matumaini yangu kwamba umepanga kuwa pamoja nasi katika masomo yetu yote yalio kwenye redio, na kwamba utawakaribisha watu wengine ili kuungana nasi tunapojifunza na kujijulisha kwa kitabu hiki ambacho ndicho cha muhimu zaidi ulimwenguni kote. Kitabu hiki ni Bibilia. Hebu sasa funga virago vyako na uungane nasi katika safari hii ambayo tuko tayari kuianza!

Vyombo Vya Wajibu Huu

Mtume Paulo anatueleza sisi kwamba njia ile ambayo twaweza kujitenga na aibu wakati Bibilia inapotajwa ni kwa kufanyika ‘Mtenda Kazi.’ Njia ya pekee ya kuifahamu Bibilia ni kwa kujifunza peke

yake. Ningelipenda kukupa changa moto tunapoanza masomo haya ya Bibilia, kwamba ujitolee kwa juhudi kuu na kwa moyo wote katika kujifunza maandiko. Kwa hakika hamna masomo yanayohitaji jitihada zaidi kuliko haya! Iwapo unataka kujifunza kwa undani zaidi masomo haya kuliko kiwango tutakacho jifunza, ni bora utafute vyombo vingine ambavyo vitakusaidia kusoma maandiko kwa undani zaidi.

Pamoja na juhudi kuu, vipo vyombo vingine ambavyo vitakusaidia katika kukuingiza zaidi katika masomo haya. Chombo cha kwanza ni dhahiri: Utahitaji Bibilia, na ikiwezekana, zaidi ya tafsiri moja ya Bibilia. Pia utahitaji kalamu na kijitabu cha kuandikia.

Kama vile kazi yeyote nyumbani hutimizwa kwa urahisi na kwa matukio bora wakati vyombo vinavyofaa vinapotumiwa itakikanavyo, vile vile masomo ya bibilia yanakuwa ya muhimu zaidi wakati unapotumia rasilmali zilizo karibu nawe. Hebu ituze juhudi hii ya kuvikusanya vyombo vinavyofaa kwa kusoma bibilia, ili kujifunza bibilia kuwe kwa ukamilifu zaidi huku ukitumia rasilmali ambazo uko nazo, nawe utashangaa jinsi masomo yako yatakavyo kuwa na tofauti kubwa.

Sura ya 1
Bibilia Na Utaratibu Wake

Maana na Kiini Chake

Kabla ya kuanza masomo ya vitabu binafsi vya bibilia, hebu tuitazame Biblia yenyewe kwa ujumla. Ni kwa nini yaitwa hivyo? Mbali na hayo, ni kwa nini wakati mwingi yaitwa “Biblia Takatifu”?

Neno Biblia latoka kwenye lugha ya ki - Latin na yamaanisha ‘Vitabu’. Hivyo basi hii ya maanisha ‘Mkusanyiko wa vitabu’ - - - sitini na sita, kwa hakika. Neno ‘Takatifu’ lamaanisha ‘Kile ambacho ni chake Mungu’ au ‘Kile ambacho cha toka kwake Mungu.’ Hivyo basi Bibilia Takatifu ni, ‘Mkusanyiko wa vitabu ambavyo ni vyake na vitokavyo kwake Mungu.’

Bibilia pia hutajwa kama Neno lake Mungu. Kwa nini? Kwa maneno yale ambayo yamenenwa nao mitume na manabii, kama Petro na Paulo. Timotheo wa pili 3:16 –17 ni mfano bora.

> Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa
> kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadhibisha
> katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda
> kila tendo jema. (Mkazo wa ziada)

Kila mara, tunathibitishiwa kwamba Bibilia siyo kusanyiko la maandiko ya kibinadamu kumhusu Mungu. Ila ni neno lake Mungu mwenyewe, lililo andikwa kupitia kalamu yake mwanadamu, yapata kama watu zaidi ya arobaini katika muda wa miaka 1500 hadi 1600. Taratibu ambayo Mungu aliyowatumia watu ili kuviandika vitabu hivi yajulikana kama *Uvuvio (Inspiration).* Neno hili lamaanisha hivi, "Kutia Pumzi ndani..." Petro analieleza hivi:

> Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali
> wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho
> Mtakatifu. (2 Petro 1:21)

Neno la Kiyunani (Greek) "Wakiongozwa." ni fanani inayoleta picha ya kuvutia. Ni neno ***Phero***, ambalo tuwalipata katika lugha ya kingereza kwa neno mtumbwi (Ferry). Hebu jifikirie kuwa katika mtumbwi huku umebebwa na mawimbi, au ukisumkumwa na dhoruba katika matanga (Sails) yake, nawe utakuwa nao ufahamu kuhusu "Uvuvio" (Insipiration), kama jinsi ile ambavyo Petro alivyo kusudia.

Taratibu Yake

Baada ya kuthibitisha Bibilia ni nini, hebu sasa tutizame jinsi ya utaratibu na mpangilio wake. Kando na yale ambayo waweza kuyatarajia, vitabu hivi havina utaratibu wa kufuatana kwa jinsi

vilivyo andikwa au kwa kulingana na mwandishi. Badala yake, taratibu yake inafuatilia mtido na ujumbe wake binafsi.

Vikundi viwili vikubwa vya vitabu ni Agano la Kale na Agano Jipya. Haikuwa hivyo hapo mwanzo, na ni kwa ajili ya sababu zilizo wazi kabisa. Katika siku zake Yesu kwa mfano, hapakuwa na kitu kama Agano la Kale na Agano Jipya. Agano Jipya halikuwa limeandikwa. Hivyo basi vitabu ambavyo vilikuwepo katika siku zake Yesu vilifahamika kama "Neno lake Mungu" au "Maandiko." Ni baada ya Agano Jipya kuandikwa na kukusanywa pamoja katika furushi moja ndipo tofauti kati ya Agano la Kale na Agano Jipya ilitokea.

Ujumbe muhimu katika vitabu vya Agano la Kale ni huu: Yesu anakuja. Hapo mwanzo kulingana na maandiko, Mungu na mwanadamu walikuwa wakishirikiana pamoja. Lakini Mungu alimuumba mwanadamu kuwa kiumbe chenye uamuzi au uwezo wa kuchagua yeye binafsi. Naye mwanadamu alichagua kumuasi Mungu. Na kwa sababu Mungu hangelivumilia uasi (Dhambi), Mungu alimuacha mwanadamu. Hivyo basi, kulikuwa na "Talaka" kati yake Mungu na mwanadamu. Talaka kati yake Mungu na mwanadamu ni ndiyo shida kuu zaidi ambayo maandiko yote yanahusika nayo.

Katika Agano la Kale, Mungu anatueleza hivi, "Je! Utaniamini nikikueleza kwamba nitafanya kitu kuhusu talaka hii"? Katika Agano Jipya, Mungu anatuambia ,
"Je! Utaniamini nikikueleza kwamba nilitenda jambo fulani kuhusu talaka hiyo?" Waweza kuona kwamba, vitabu vya Agano la Kale vya sema kwamba Yesu anakuja, na yakuwa atapatanisha talaka kati ya Mungu na viumbe vyake. Agano Jipya yatueleza habari hii njema: Yesu alikuja, na Yesu alipokuja aliipatanisha talaka kati yake mwanadamu na Mungu.

Mbali ya mgawanyiko huu mkubwa wa Agano la Kale na Agano Jipya, ipo migawanyiko katika kila Agano. Vitabu vya Agano la Kale vimo chini ya vikundi tofauti.

Kwanza, vimo vitabu vitano kuhusu Sheria. Katika vitabu hivi, Mungu atueleza yale yaliyo mema na yale yaliyo maovu, huku akitupatia Kiwango chake cha utakatifu.

Vinavyofuata ni vitabu kumi vya Historia, ambavyo hutueleza kwamba, wakati mwingine watu wake Mungu waliyatii yale

yaliyokuwemo katika vitabu vya Sheria na wakati mwingine hawakuyatii. Hadithi zao zatumika kama mfano kwetu.

Vitabu vya historia vimefuatiliwa na vitabu vya Mashairi. Katika vitabu vya mashairi Mungu anazungumza kwa mioyo ya watu wake wanapojaribu kuishi kulingana na Neno lake katika ulimwengu huu. Kwa mfano, umuhimu mkuu zaidi wa kitabu cha Ayubu ni kuwalenga watu wanaoteseka. Nacho kitabu cha Zaburi cha husu kuabudu. Kitabu cha Methali kinatueleza kuhusu jinsi ya kuhusika na kushiriki na watu wengine.

Kila kimoja cha vitabu hivi kina funzo au mawaidha ya kuwatia moyo na kuwapatia ujuzi wa kimaisha wake wanaoamini.

Sehemu inayofuata ndiyo kubwa zaidi ya katika Agano la Kale.Hii ni ya Manabii. Sehemu hii imegawanywa kati ya Manabii Wakuu na Manabii Wadogo---Kugawanywa huku hakuambatani na umuhimu wa ujumbe ila ni kulingana na ukubwa wa kitabu kile. Kwa hakika, ni lazima tukumbuke kwamba ilichukua muda mrefu kwa manabii wakuu kusema maneno hayo yote! Na hivyo walihitajika kufahamika kwa kutofautishwa kwa njia fulani.

Navyo vitabu vya Agano Jipya, vimegawanywa kwenye sehemu tano. Kikundi cha kwanza kina vitabu vitabu vinne. Hivi ni vile vyinavyohusu hadithi ya maisha yake Yesu Vitabu hivi vyajulikana pia kama vitabu vya Injili. Vimeandikwa na Mathayo, Marko, Luka na Yohana.

Kifuatacho ni kitabu cha Matendo ambacho ni kitabu cha Historia. Hiki chafuatwa na Nyaraka, au Barua. Hivi vimo katika vikundi viwili: Nyaraka za Paulo na Nyaraka za kijumla. Nusu ya Agano Jipya ni nyaraka zilizoandikwa na Mtume Paulo kwa makanisa yaliyokuwa machanga na yaliyoundwa baada ya ufufuo wake Yesu. Nyaraka zingine ziliandikwa na watu kadha wa kadha. Mwisho, kipo kitabu kimoja cha Unabii ambacho chaitwa Ufunuo.

Tunapoanza kusoma Bibilia, twastahili kusoma agano la kale tukitambua kwamba ujumbe mkuu wa Agano la Kale ni: *Yesu anakuja.* Huu ndiyo ujumbe mkuu katika Agano la kale. Nayo Agano Jipya ujumbe wake ni: *Yesu alikuja.* Huu ndio ujumbe mkuu katika Agano Jipya.

Sura ya 2
Biblia, Kusudi Lake, Uandishi na Asili Yake

Kusudi Lake

Kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, shina kuu ya biblia yumhusu Yesu Kristo. Watu wengine hufikiri kwamba Bibilia ni kitabu cha maelezo kuhusu maisha bora; watu wengi hufikiri kwamba Yesu alionyeshwa tu kama mwalimu na mfano bora wa kuishi. Yesu Kristo ndiye shina kuu katika bibilia yote. Tunapo tilia mkazo kuhusu wazo hili ni lazima tukumbuke kwamba Bibilia inazo kusudi nne kubwa. Nazo kusudi hizi nne ni:

a. Kumuonyesha Yesu Kristo kama Mwokozi na mkombozi wa ulimwengu huu. Ili sisi tufahamu kusudi hili la kwanza, twahitajika kufahamu kwa sababu gani Mwokozi anahitajika.

b. Na hivyo basi, sababu ya pili ya Bibilia ni kutufahamisha utangulizi wa historia ya nyakati za Yesu.

Walakini, tunapofikia Mwanzo 12, hadithi inaanza kusonga pole pole. Kutoka katika sura hii hadi kitabu cha Ufunuo – sura zote 1,178 zilizobaki – hoja ya hadithi inaanza kuwa nyembamba. Kutoka hapa, hadithi yamhusu Ibrahimu na uzao wake; na hasa uzao wake mmoja ambao mataifa yote ya ulimwengu yangalibarikiwa kumpitia yeye, Masihi, Yesu.

Wakati tunapo fahamu kusudi hizi mbili za kwanza, za pili zinazosalia zinakuwa zinakuwa dhahiri kabisa. Nazo ni:

c. Kumuongoza yeye asiyeamini ili aamini;

d. Kumuongoza muamini ili apate utakaso.

Uandishi Wake

Ni nani aliyeviandika vitabu vya Biblia? Vilandikwa wakati gani na viliandikwa wapi? Ni ligha ipi au zipi ambayo biblia iliandikwa? Je! Zipo nakili zo zote za kwanza ambapo zipo hadi siku ya leo? Ni nani aliye fanya uamuzi wa kuvikusanya vitabu hivi na

kuviweka katika taratibu iliyopo siku ya leo? Hauhitaji kuisoma Bibilia kwa wakati mrefu kabla ya maswali haya kutukia katika mawazo yako. Hebu kwanza tufikirie kuhusu Uandishi wa Bibilia. Tangu mwanzo tumesema kwamba Mungu ndiye mwandishi, kupitia kalamu za watu (tutazungumzia kuwahusu hawa watu hapo baadaye). Lakini kwanza, yapo maneno mawili yanayohitajika kufafanuliwa na kufahamika vyema wakati tunaposema kwamba Mungu ndiye aliyeviandika vitabu hivi. Neno la kwanza ni **Ufunuo.** Ufunuo ni neno linalotumika kwa njia tofuati kuhusu jinsi Mungu anavyo dhihirisha kweli kwake mwanadamu – kupitia kwa maumbile ya asili, kwa kumpitia Roho Mtakatifu, na kwa kupitia njia nyingi. Neno lingine ni **Uvuvio** (Inspiration). Hii inamaanisha kile wasomi wa elimu ya dini (theologia) wanakitaja kama "Ufunuo Makhususi." Bibilia ni ufunuo makhususi wake Mungu. Ina mwanzo na mwisho. Kwa kipindi cha muda wa miaka 1600 Mungu aliwaongoza watu katika kuviandika vitabu hivi. Lakini kwa wakati huu huo ufunuo makhususi au Uvuvio umekoma, na hautumiki tena.

Baada ya kudhibitisha kwamba Mungu ndiye aliye viandika vitabu vya Bibilia, ni lazima pia tuongezee kwa kusema kwamba watu waliviandika hivi vitabu. Hawa watu walikuwa ni Wafalme, Wavuvi wa Samaki, Wachungaji wa kondeni, Wakuu wa majeshi, na wakuu wa kisiasa. Mmoja alikuwa Tabibu (Daktari) na mwingine Mtoza Ushuru- yaani watu wa namna mbali mbali.

Asili yake

Ni nani aliyefanya uamuzi wa yale ambayo yahitajika katika bibilia, na wakati gani? Na uamuzi huu ulifanyika vipi?

Uamuzi huu ulituwa miaka100 baada ya kuzaliwa kwake Kristo. Katika Baraza kuu la Jamnia, Agano la Kale lilikusanywa kirasmi, ingawaje ilikuwa imetumika kwa zaidi ya miaka mia tatu au mia nne. Vitabu hivi vilikusanywa na kuunganishwa pamoja kulingana na kuaminika kwao waandishi wa kibinadamu na sifa zao kama manabii au waandishi. Vingi vya vitabu hivi vilikuwa wimeandikwa katika lugha ya Kihebrania.

Navyo vitabu vingi vya Agano Jipya, viliandikwa kwa lugha ya Kiyunani (Griki). Hivi navyo vilikusanywa katika mwaka wa mia sita

na tisini na mbili baada ya kuzaliwa kwake Yesu. Katika Baraza Kuu la Trullan. Kipimo ambacho kilitumika kuvichagua vitabu hivi chajulikana kama ***Canonization,*** yaani Kanuni ya Vipimo. Vifuatavyo ni vipimo na kanuni zilizotumika: Je!-

1. Kitabu hiki kiliandikwa naye Mtume au mtu aliyekuwa wa karibu na mtume?
2. Kitabu hiki kinao ujumbe ambao waweza kumlisha na kukutana nayo mahitaji yake anaye amini?
3. Je, Vitabu hivi vyalingana na kuwa na umoja na vitabu vingine kwenye bibilia?

Ilikuwa aje kwamba vitabu vingi vilivyo andikwa miaka mingi aliyopita bado vipo hata siku ya leo? Vimetunzwa kwa uangalifu mwingi. Kwa hakika, hatuna nakili za kwanza za maandiko haya; makaratasi hayawezi kudumu kwa muda mrefu mno. Hata hivyo zipo nakili nzuri, na uangalifu mkubwa ulitumika katika tafsiri ya nakili hizo hadi lugha ya sasa.

Kumalizia

Je! Mtu awezaje kuthibitisha kwa uhakika kwamba Bibilia ni Neno la Mungu lililovuviwa? Twaweza kufahamu kwa njia gani kwamba vitabu vilivyochaguliwa ni vile vilivyotakikana? Ipo tu njia moja ya kufahamu haya. Naye Yesu anatueleza ni njia ipi. Alisema, “kama mtu akitaka kufanya, atafahamu.” Inapatikana katika moyo wako.

Unapolijia neno lake Mungu kwa nia ya kutaka kutenda kile linalosema, unapofanya yale unayoyapata pale, hiyo huyafanya mabadiliko makubwa mno katika maisha yako, hivi kwamba utasema, “Hilo ni neno lake Mungu. Ni lazima liwe. Hapawezi kuwa mijadala ya kuthibitisha ukweli mwingine.”

Maswali ya Somo

1. Kusudi nne za Bibilia ni zipi?_____

2. Bibilia inamuongoza muwamini kwa kazi njema kivipi?_____

3. Wakati wa kuufanya uamuzi, Je! Ni Ufunuo wa kibinafsi au ni Ufunuo Makhususi ulio wa muhimu?_____

4. Zitaje kanuni au vipimo vilivyo tumika katika kuvichagua vitabu vya Agano Jipya? _____

Sura ya 3
Jinsi Ya Kuisoma Bibilia

Tunapofikia wakati wa kuisoma Bibilia, twahitajika kuwa waangalifu na wenye busara. Taratibu moja iliyo bora katika kujifunza ni ile ya: **Kutizama**, **Kutafsiri** na **Kutenda.**

Kutizama ndiko kwa kwanza. Unaposoma fungu la maandiko, wajiuliza swali hili, “Fungu hili lasema nini?” Hatua inayofuata ni Kutafsiri, hapa unauliza swali hili, “Fungu hili la maanisha nini?” Halafu Kutenda kwafuata. Katika hatua hii, wastahili kuuliza swali hili, “Fungu hili laamanisha nini kwangu mimi?”

Kufahamu yale ambayo maandiko yanayosema na yale yanayo maanisha ni muhimu. Lakini usipoyatenda yale fungu lile linasema, kujifunza kwako hakuna maana ye yote ile. Unapofikia hatua ile ya “kutenda,” unatafuta maana ya fungu lile la maandiko kwako binafsi kwa kulifanya hilo swali la ujumla kuwa ni la kipekee. Yajaribu haya maswali ili kukusaidia unapoanza kujifunza:

- Je! Ipo mifano ye yote ya kuigwa?
- Je! Yapo maonyo ye yote ya kuwa mwangalifu nayo?
- Je! Ipo amri ye yote inayohitajika utii?
- Je! Zipo dhambi zo zote zile zinazohitajika kuachwa?
- Je! Zipo kweli mpya kumhusu Mungu na Yesu Kristo?
- Je! Zipo kweli mpya zingine kuhusu maisha yangu binafsi?

Wakati unapojifunza Bibilia, zipo sheria muhimu ambazo zahitajika kutiliwa maanani. Mojawapo ni; unapofikia fungu la maandiko, kumbuka hivi- hata kama ipo tafsiri moja peke yake, yawezekana kuwepo na njia nyingi zaidi za kuitumia au kutenda ile tafsiri. Waweza kutilia mkazo fungu la maandiko fulani katika maisha yako, tafadhali mruhusu Roho Mtakatifu kuitenda kazi tofauti maishani mwa mtu mwingine kupitia andiko hilo.

Pili, kwa sababu Bibilia ni kitabu kuhusu Kristo, watakikana kumtafuta Kristo wakati wote unapojifunza maandiko. Tatu, unapofikia fungu la maandiko linalo shangaza ama lisilofahamika vyema, tafsiri fungu hili kwa kulinganisha na vifungu vingine ambavyo vinatambulikana vyema zaidi. Vipo vifungu vingi ambavyo ni vigumu kuvifahamu. Na pia vipo vifungu vingine vingi ambavyo ni rahisi kuvifahamu. Tegemea vifungu vile vilivyo vyepesi kuvifahamu katika kukuongoza kutafakari kuhusu vifungu vilivyo na ugumu.

Lingine la muhimu ni: Usiingilie kifungu cho chote kile huku ukiwa tayari umeufanya uamuzi kuhusu maana yake. Waweza kuwa sawa kabisa katika kufikiria kwako kuhusu maana unayopatia kifungu kile, na pia yawezekana kwamba waweza kukosea! Itakuwa ni vigumu kwake Roho Mtakatifu kukufundisha kama tayari umeufanya uamuzi kuhusu yale unayoyafahamu.

Kanuni ya nne iliyo muhimu, hasa kama wewe wafundisha maandiko, ni katika kutii mwongozo wa maandiko kabla ya kumfunza mwingine.

Nayo kanuni ya tano hii. Wakati wote kumbuka kwamba Mungu huzungumza nasi kupitia neno lake. Hivyo basi likaribie Neno la Mungu kwa uangalifu, huku ukimwomba Mungu akufunulie mambo ya kibinfasi kumpitia Roho Mtakatifu.

Dokezo lingine ni hili: Wakati wowote ule, tilia maanani yale yote yaliyo kwenye kifungu cho chote kile. Kama mtu ashawahi kukunakilia bila ya ufahamu wa yote yale uliyoyasema, lazima uligundua kwamba maneno yaweza kubadilishwa na kuwa na maana tofauti tokana na ile uliyoitumainia kuwepo mwanzo. Vivyo hivyo, maandiko yaweza kutumiwa kuthibitisha cho chote kile kama ukibagua vifungu na kuvitoa katika mazingara yake. Kwa hakika

ukijifunza msitari mmoja kando na mistari mingine, utapotoshwa na tafsiri yake.

Na sasa baada ya kuudhibitisha msingi wa jinsi ya kujifunza neno lake Mungu, tutajitosa kwenye kitabu cha kwanza, Mwanzo. Tunapoanza, ombi langu kwako ni kwamba uingie ndani mwa Neno la Mungu. . . na kuliruhusu Neno lake Mungu kuingia ndani mwako

Maswali ya Somo

1. Taratibu njema ya kuisoma Bibilia ni ipi?_____

2. Ni lipi litakalo kusaidia kufahamu vyema vifungu vigumu vya Maandiko? _____

3. Ni jambo gani unalostahili kumuuliza Mungu kabla ya kujifunza
   Maandiko?_____

Sura ya 4
Mwanzo – Kitabu cha Mianzo

Kitabu cha Mwanzo ni kuhusu mianzo. Neno Mwanzo la maanisha hasa “Kuanza.” Kitabu hiki ndicho Mwanzo wa Bibilia, na pia ni kitabu kuhusu mianzo. Mwanzo wa kwanza unaoelezwa ni ule wa ulimwengu.

Katika kitabu cha Mwanzo, Mungu anatueleza kumhusu mwanadamu, kama jinsi alivyokuwa hapo mwanzo na kama alivyo sasa. Hili litatusaidia sisi kujifahamu wenyewe. Anatuambia kuhusu dhambi. Tukitizama jinsi dhambi ilivyotukia tutafahamu jinsi inavyo husika nasi leo. Anatuonyesha mawasiliano yake ya kwanza na mwanadamu, na mazungumzo haya yanatusaidia sisi kufahamu jinsi anavyo husika nasi pia. Katika utata kati yake Kaini na Habili, twaona jinsi matata yanavyoanza, na tunaanza kufahamu utata au pingamizi tulizo nazo siku ya leo.

Katika sura ya sita hadi ile ya tisa, twasoma kuhusu janga la kwanza ulimwenguni. Nalo ni gharika kuu. Katika hadithi hii,

twaupata mfano wa wokovu. Kwa ajili imani yake Nuhu, Mungu alimwokoa tokana na uharibifu. Hata sisi tukiwa na imani, twaweza kuokolewa tokana na uharibifu wa dhambi.

Katika kitabu hiki chote twaipata hadithi baada ya nyingine inayotuonyesha kwamba Mungu ndiye huyaongoza mambo yote. Baada kurudiwa kwa funzo hilo, twaweza kuwa na shaka kwamba Yeye ndiye anayaongoza mambo yote hata siku ya leo?

Wajibu wako leo, ni uanze kukisoma kitabu cha Mwanzo. Na unapofanya hivyo, jiulize maswali haya: Hili lasema nini kuhusu mambo yalivyokuwa hapo awali? Hili la maanisha nini tukilinganisha na jinsi mambo yalivyo siku ya leo? Na hili la zibadilisha fikira zangu kwa njia ipi?

Maswali ya Somo

1. Ni nini katika kitabu cha Mwanzo kinachotusaidia sisi kufahamu ulimwengu siku ya leo?_____
2. Ni kwa sababu gani Mungu alimwokoa Nuhu kutoka kwa uharibifu?_____
3. Waweza kumuuliza Mungu aumbe nini ndani yako?_____ _____

Sura ya 5
Uumbaji ni Kweli?

Kitabu cha Mwanzo – kwa hakika, Bibilia nzima – yaanza na hadithi ya Uumbaji.

Pamoja na ukuu wa kweli hiyo, hadithi hii yachukua sura moja na nusu peke yake. Kwanini iwe hivi? Jinsi tulivyo jadili kwenye sura iliyopita, kitabu hiki kiliandikiwa siyo kueleza jinsi mambo yalivyokuwa tu, bali kwamba tufahamu jinsi mambo yalivyo. Mungu hana wajibu kwetu ili kueleza jinsi kulivyokuwa. Na hahitaji kujitetea mwenyewe. Kusudi lake siyo kuthibitisha elimu ya uumbaji, ila kuthibitisha kweli ambazo hutusaidia sisi kumfahamu Yeye pamoja na uhusiano wake kwetu sisi.

Hata hivyo hatuwezi kukipitia kitabu hiki bila ya kujadiliana jambo ambalo ni lazusha mijadala mingi kuhusu Bibilia. Yapo mawazo mawili yenye ubishi katika habari za uumbaji. Kwanza, lipo wazo ambalo msimamo wake ni kwamba habari hizi za uumbaji hazilingani na mafundisho ya kisayansi, na kwa sababu hiyo Bibilia haiwezi kuwa ni
Neno la Mungu lililo vuviwa. Kwa upande mwingine, ubishi unapinga swali hili. “Bibilia yaweza kutegemewa kisayansi?” Wale ambao huwa na msimamo huu husema, “Bibilia haimo hukumuni bali sayansi ndiyo imo katika hukumu.”

Jambo kuu ni hili: Je! Bibilia na Sayansi zalingana kuhusu jinsi ulimwengu ulivyo uumbika?

Twahitahiji kuweka mambo fulani katika mtizamo bora. Jambo la kwanza, asili na misingi ya sayansi hairuhusu kuwa nayo fursa kuhusu imani katika Mungu. Hii si kusema kwamba wanasayansi hawawezi kuwa Wakristo. Sayansi ni elimu kuhusu mambo ya hakika au matukio yakufanyiwa uchunguzi na kupimwa kwa makadirio yanayoweza kuthibitishwa. Misingi yake ni utafiti na kukadiria jinsi ya mambo, kujumulisha na kutenda mambo. Sayansi huongozwa. Asili yake Mungu, ni kwamba Mungu hawezi kupimwa au kukadiriwa au kuwa chini ya elimu ya ututafiti kama huo. Haiwezekani kumkaribia Mungu kupitia taratibu ya kisayansi. Njia ya kumwendea Mungu na ya kipekee ni Imani. Twaelezwa haya katika kitabu cha Waebrania 11:6 kinapotuambia:

> “Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamfuatao.”

Tulisoma, “Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi” (Mwanzo 1:1). Kisha twaendelea kusoma hivi “Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza ilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji.”(v.2).

Bibilia yasema, Roho wa Mungu ikatulia juu ya uumbaji na kuendeleza na kubadilisha. Kwa mfano, Mwanzo 1:9 yasema,

> “Halafu Mungu akasema, “Hebu maji yaliyomo chini ya mbingu yakusanyike katika mahala pamoja, na ardhi kavu **itokee**.” (mkazo umeogezwa)

Mungu hakusema, “Hebu nchi kavu na itokee.” Huu siyo wakati ambapo nchi kavu ilipo uumbwa. Ni dhahiri kwamba tayari ilikuwa imeumbwa, lakini ilikuwa chini ya maji. katika msitari huu, inafunuliwa. Ni jambo la kusisimua kwamba jamii ya kisayansi yaamini kwamba ulimwengu wote ulikuwa chini ya maji hapo wakati mmoja.

Neno **bara**, au “Uumbaji,” la maanisha kutengeza kitu kutoka kwa utupu. Maneno mengine kati ya msitari 2 na 20 ni tofauti. Ni maneno yanayoeleza kubadilika, kuchukuwa kitu na kubadilisha maumbile yake. Tunapolijia neno hili **bara**, au uumbaji, linatukia katika maji.

> “Mungu akaumba nyangumi wakubwa, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho, ambavyo maji yalijawa navyo kwa wingi kwa jinsi zao, na kila ndege arukaye, kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema.” (Msitari 21)

Kwa mara nyingine pana ukubaliano kati ya wanasayansi pamoja na Bibilia. Wanasayansi waonekana kuwa na uhakika kwamba uhai wa maumbile ulitoka majini, na haya ndiyo maandiko katika kitabu cha Mwanzo yanayosema.

> Tendo lingine la **bara** latukia katika msitari 27:
> “Naye Mungu akaumba mwanadamu katika mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamuke aliwaumba.”

Hadithi ya Uumbaji katika kitabu cha Mwanzo yaeleza mwanzo wa mambo ulimwenguni. Hata baada ya matukio haya ya uumbaji, Roho wa Mungu aliendelea kubadilisha na kuendeleza maumbile. Haya yanalingana na yale wanasayansi wanayoyatambua kuhusu taratibu ya uumbaji, hapa hamna ubishi kati ya bibilia na wanasayansi. Hata hivyo, waaminio uumbaji (Creationists) nawanaamini katika mageuzi na mabadiliko ya maumbile (Evolutionsists), hutofautiana kimawazo wanapozungumza kuhusu maswala matatu yasiyo eleweka kisayansi. Walakini, kitabu cha Mwanzo katika bibilia ina maelezo haya. Jibu ni dhahiri. **Bara** – Mungu aliumba.

Maswali ya Somo

1. Je! Ni bora kujifunza kuhusu Mungu kupitia Sayansi au kupitia Imani? _____

2. Ni maswali yapi matatu ambayo Mwanzo inajibu ambayo sayansi haiyajibu?_____

3. Bibilia ni kitabu cha aina gani?
   _____

Sura ya Sita
Kuzaliwa kwa Binadamu

Tayari tumejadiliana kuhusu mwanzo wa ulimwengu huu, sasa hebu tuzungumzie kuhusu sisi binafsi. Katika sura hii, tutatizama yale ambayo kitabu cha Mwanzo kinayo zungumzia kuhusu mwanzo wake mwanadamu. Kumbuka kwamba, kusudi la kitabu cha Mwanzo ni kutueleza jinsi ilivyo kuwa ili tuelewe jinsi ilivyo. Tunapofikia somo kuhusu mwanzo wake mwanadamu, tunakaribia somo linalotuhusu sisi. Je! Kitabu cha Mwanzo kina lipi la kutuambia kuhusu kusudi lake Mungu katika uumbaji wa mwanadamu? Hebu tuanze kwa kusoma jinsi mwanaume na mwanamke walivyo tokea kuwa.

> "Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; . . . (Mwanzo1:26-28a)
>
> Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. . . (Mwanzo 2:18)

Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama pahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. (Mwanzo 2: 21-24)

Katika mfano wa Mungu

Kitu kinacho vutia zaidi katika kifungu hiki ni kwamba mwanadamu aliumbwa katika mfano na sura yake Mungu. Maneno haya ni ya kutambulikana kwetu. Walakini , hii yamaanisha nini? Kwa kuwa Mungu ni Roho, yeye hana mwili, na hivyo basi hii haimaanishi jinsi tunavyo fanana sisi. Maana yake ni hali ile ya uwezo wake mwanadamu kuwa wa kiroho. Na hii ndio njia ambayo sisi twafanana naye Mungu. Hata hivyo katika Mwanzo 3, twaona kufanana huku kati yetu naye Mungu kuliharibiwa na dhambi ya bina damu. Kwa ajili ya hali hiyo, shida kuu ambayo maandiko yanakumbana nayo ni katika "Uumbaji mpya" mfano wake Mungu ndani yetu. Mwanzo 2 watuonyesha mwanadamu alivyo umbwa na jinsi alivyotarajiwa kuwa. Mwanzo 3 waonyesha jinsi mwanadamu alivyo.

Mwanamume na Mwanamke

Jambo lingine linalojitokeza kuhusu uumbaji wa mwanadamu ni kwamba yeye alimwumba mwanamume na mwanamke. Huu ndio mfano wa kwanza kuhusu upasuaji kwa njia ya dawa ya kufa ganzi (lala). Daktari wa kwanza wa dawa za kufa ganzi alikuwa Mungu. Mungu alimfanya Adamu kupatwa na usingizi mzito. Kisha akauchukua ubavu mmoja na kumfanya mwanamke. Ishara iliyo hapa ni ya kuvutia mno. Mungu hakumtoa mwanamke kutoka kwenye kichwa chake mwanamume ili amtawale, na hakumtoa katika miguu yake ili kwamba akamtumikie yeye. Alimtoa mwanamke kutoka katika upande wake mwanamume, ili kwamba awe karibu na moyo wake.

Kwa nini Mungu alimwuumba mwanamke? Neno la Kiebrania "**Pekee**" laweza kutafsiriwa zaidi kama "Upungufu." Neno hili "msaidizi" laweza kutafsiriwa kama "Mkamilishaji." Kama ukitizama sarufi ya lugha ya Kiebrania, utatambua kwamba wakati Mungu alimleta huyu mwanamme na mwanamke pamoja katika hali ile tunayoitaja kama 'Ndoa takatifu," au kuja pamoja kimwili, huyo mwanamume na mwanamke waliungana katika mwili moja na kufanyika kuwa mwanadamu kamili.

Ni jambo la muhimu kutambua kwamba wakati Mungu alimleta mwanamume na mwanamke yule pamoja, alileta ushirika muhimu mno katika amri iliyo ya asili zaidi ulimwenguni. Shirika hili laitwa jamii. Ulikuwa mpango wa Bwana kuumba mwanamume na mwanamke ili kuwaunganisha watu hawa wawili ili wawe wazazi. Nao waweze kumlea mtu ambaye atakuwa na awe mzazi pia. Huu ndio muelekezo mkuu wa maisha ambao unaleta kuzaliwa, kulewa na kupata mwelekeo maishani kwa kizazi chote cha binadamu.

Ulikuwa ni mpango wa Mungu kuwaunganisha mwanamume na mwanamke katika hali ya ushirika ili kwamba wafanyike kuwa wazazi. Hii ndiyo maana Mungu alimuumba mwanamme na mwanamke. Iwapo Mwanamme ana ushirika wa karibu na Mungu naye, mwanamke vile vile, hawa wawili wanapomsongea Mungu, uhusiano wao unakuwa wa karibu zaidi kati yao wenyewe.

Unapojifunza kuhusu ndoa katika kitabu cha Mwanzo, utatambua kwamba huu ni uhusiano wa kipekee katika njia mbili. Kwa sababu ya ndoa, mwanamume, atamwacha baba yake na mama yake. Yeye hujitenga mbali na jamii yake ambayo alikuwa nayo kwa miaka ishirini au ishirini na tano. Na pia kwa sababu ya ndoa, yeye atawaacha wote wale. Yeye atakikana kujitolea mhanga kwa sababu ya mwenziwe katika ndoa kwa maisha yake yote. Hili ndilo kusudi lake Mungu.

Mpatie Mungu ushirika wako na mwenzi wako pamoja na uzazi wenu. Mruhusu yeye aijenge nyumba yako nayo itakuwa dhabiti.

Sura ya 7
Je! Wewe Upo Wapi?

Mojawapo ya sehemu inayotambulika mno katika kitabu cha Mwanzo yapatikana katika sura ya tatu, ambapo Adamu na Hawa wana kula tunda walilokatazwa. Sura ya 2 ilituonyesha mwanadamu, jinsi alivyoumbwa na jinsi alivyofanyika kuwa alivyo leo. Sura hii yatuonyesha dhambi – ilivyokuwa wakati ule, na ilivyo leo. Inawaonyesha Adamu na Hawa wakikabiliana na uchaguzi mmoja ambao sisi hukumbana nao wakati mwingi kila siku: Je! Tutatenda jinsi tunavyo kusudia au jinsi Mungu anavyo tutarajia sisi kufuata njia yake? Mungu alitufanya kuwa viumbe vyenye uchaguzi. Kwa ajili hii, twaweza kutenda mapenzi yake Mungu, au kutoyatenda.

Sura ya tatu ya Mwanzo inaeleza kuhusu upotovu uliotokea mara ya kwanza. Inaeleza mvutano wa hisia kuhusu uchaguzi ili kwamba tupate kuelewa jinsi hali hiyo ilivyo. Tukio hili tulielezwa hapo mwanzo, katika sura ya 2:8-9.

> Bwana Mungu akapanda bustani upande wa mashariki wa Edeni, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya. Bwana Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

Kwa sababu isiyotambulika watu wamekuwa na wazo kwamba tunda hili ni lile Tofaa (apple) kama pera hivi, lakini hamna tunda linalo tajwa, katika mistari hii au katika sura ya tatu. Badala yake, twasoma kuhusu mti wa uzima, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

Kabla hatujaendelea mbele, twahitaji kuzungumzia kuhusu lugha inayotumika mahala hapa. Hadithi hii ni ya kihistoria, lakini pia ni ya methali au mfano. Methali ni hadithi ambayo watu, mahala, na vitu vinayo maana kando na historia au maana halisi iliyo dhahiri, na kwa wakati mwingi huwa ni hadithi ya kuongoza katika kurekebisha tabia.

Katika maelezo kuhusu bustani ya Edeni, namna ya miti ambayo yaelezwa yaonyesha kwamba Mungu alikuwa akutane na mahitaji yake mwanadamu mahala hapo. Hebu tizama umuhimu wa utangulizi: kwanza kabisa, miti hii ilikuwa itosheleza mahitaji ya macho ya mwanadamu. Kisha kukutana nalo hitaji lake la chakula, na

baadaye kumpa yeye uhai. Na pia kulikuwepo mti wa ujuzi wa mema na mabaya, na hawakuhitajika kula kutoka katika mti ule.

Katika sura ya tatu, ambapo hadithi ya kuhusu dhambi ya kwanza ilipotukia, gundua kwamba taratibu ya umuhimu inabadilika. Badala ya kuweka macho mbele, chakula pili, uzima tatu na ujuzi usikuwepo, wao wanaweka chakula kwanza, kisha macho, na baadaye ujuzi – wao hawakaribii uzima. Badala yake wao walikumbana na mauti ya kiroho.

Kumbukumbu la Torati 8:3 yatueleza kwamba "Mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana." Sisi hatuishi tu kwa kuwa sisi hutoka na kutizama njia za kukutana na mahitaji yetu au kutosheleza tamaa zetu tu. Kuishi kwa kweli hutokana na kumtii Mungu.

Wakati Mungu alipomweka Adamu na Hawa katika bustani la Edeni, aliwapatia vyote walivyo vihitaji. Waliyafahamu mahitaji yao kwa kuwa yeye ndiye aliyewaumba. Na kwa kuwa yeye ndiye aliyetuumba sisi, anayafahamu mahitaji yetu pia; na makusudio yake yote ni kwamba atakutana na mahitaji yetu.

Hapa, waweza kushangaa ni kwa sababu gani macho yanakuwa ni ya kutangulia katika taratibu au ngazi ya umuhimu. Wakati maandiko yanapozungumza kuhusu macho, haimaanisha macho haya ya kawaida; kwa mfano, katika Mathayo 6:22-23, Yesu asema, "Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na nuru. Lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa giza, basi ile nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza; si giza hilo!" Yesu hakuwa akizungumzia kuhusu maono ya kimwili. Alikuwa akizungumzia kuhusu tunavyotizama mambo, hali ya nia yetu, mtizamo wetu katika maisha. Na wakati Mungu alipoweka hili katika hatua ya mbele ya yale yaliyo ya kuvutia katika bustani la Edeni, yeye alikuwa akisema kwamba, wao walihitajika kumtizama yeye ili kwamba akutane nayo mahitaji yao.

Imo picha nyingine katika sura hii pia, Baada yake Adamu na Hawa kuanguka katika dhambi,

"Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone. Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi?" (msitari 8-9)

Ni jambo la kuvutia kuona kwamba Mungu anaanza mazungumzo naye Adamu na Hawa kwa kuuliza maswali: “Uko wapi? Ni nani aliyekuambia kwamba upo uchi? Je! Umekula kutoka katika mti?” (msitari 9, 11). Mungu alikuwa tayari anayafahamu majibu yale; Yeye yupo kila mahali wakati wote, na alikuwa akiyaona yote. Mungu aliyauliza maswali haya kwa sababu ya mambo ambayo Adamu na Hawa hawakuyafahamu. Maswali haya yalibuniwa ili kwamba wapate kufikiria. Fahamu kwamba wakati Mungu alipo uliza, “Uko wapi?” kwa hakika alikuwa akisema, “Mbona unajificha mbali nami?”

Baada ya Adamu kukiri kwamba yeye alikuwa akijificha kwa kuwa alikuwa uchi, Bwana anamuuliza swali la pili ambalo ni muhimu mno: “Nani aliyekuambia kwamba upo uchi? (Msitari 11a) katika lugha ya kiebrania, swali hili lasomwa hivi, “Ni nani aliyekufanya wewe kufahamu hayo?” Swali halisi, ni kwamba Mungu alikuwa Yeye ndiye kina cha habari hizo. Zipo habari ambazo Yeye atutaka sisi kuwa nazo, na zingine huchagua kutotufahamisha sisi, lakini hamna habari ambazo Yeye hazifahamu mwenyewe.

Mungu analiuliza swali lingine, “Je! Ulikula kutoka mti uliokatazwa?” (msitari 11b). Adamu na Hawa walikuwa wamekosa kumtii Mungu. Sasa walikuwa wakijificha kichakani, huku wakijifunika na majani ya mti katika miili yao na kuteseka katika tukio la kuasi kwao. Kama wewe washerehekea katika matokeo ya kuasi kwako utafahamu kwamba ni jambo la kuchukiza. Hebu jiulize swali hili: Umekuwa ukila kutoka katika mti uliokatazwa? Umekuwa mtu wa kutokulitii neno lake Mungu, au kupuuza mwongozo wake katika maisha yako?

Swali la nne lake Mungu, “Je! Umefanya nini?” linaelekezwa kwake Hawa, na linazalisha kukiri, hata kama yafuatana na kujitetea kwa visababu. Neno Kukiri lamaanisha kukubali. Toba ya maanisha kukubaliana naye Mungu kuhusu yale uliyoyatenda. Mungu alimtaka Hawa kuyaweka wazi na peupe yale yaliyotokea kati yao, ili wakabiliane nayo. Vile vile, haya ndiyo ambayo anataka kutoka kwetu sisi. Atutaka sisi tutambue yale tuliyoyatenda na kukabiliana nayo kwa uaminifu.

Mwanzo 3 ni kifungu cha kihistoria na kimethali. Ni picha yao watu wawili ambao wametenda dhambi na jinsi Mungu alivyo

kabiliana nao. Mbali na hayo ni picha yetu sote ambao tumetenda dhambi na jinsi Mungu anavyo kabiliana sisi. Ni picha kuhusu dhambi na matokeo ya dhambi ile. Pia ni picha yake Mungu akimtafuta mwenye dhambi na kuzifungua njia za mawasiliano.

Sura ya 8
Ndugu yako Yupo Wapi?

Mojawapo wa jumbe zililizo kuu katika Bibilia, ni hitaji la mwanadamu kupatanishwa na Mungu. Yeye huanza kufanya upatanisho mara tu dhambi inapotendwa. Katika Mwanzo 3:15, unabii wa kwanza wa kimasihi watokea wakati Mungu anapozungumza naye Nyoka.

"Nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huyo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino."

Huku tukifahamu kwamba nyoka anamwakilisha shetani, hapa ndipo kwa mara ya kwanza twamuona Mungu akidokeza kuwa atamleta mtu ulimwenguni ambaye atayarekebisha mambo. Hili ni tukio bora lililotokana na dhambi ya Adamu na Hawa.

Lakini kulikuwepo na matokeo mengi maovu! Kwanza, mwanadamu alitenganishwa kutoka kwa Mungu. Kisha katika sura ya 4 twasoma kuhusu tukio lingine la kuanguka kwake mwanadamu – Kutofautiana. Mungu anaeleza kutofautiana kama kulivyo kuwa ili tuelewe jinsi ilivyo leo. Sisi hutofautiana kibinafsi, na wenzi wetu, na watoto wetu na wazazi wetu. Kutofautiana hutokea katika mahali petu pa kazi, na pia kupo kutoafuutiana kwa kimataifa. Kutofautiana ndiyo shida yetu kuu zaidi. Katika Mwanzo 4, tutagundua misingi kadha ambayo husababisha shida hii pamoja na suluhisho linalo tatua. Anatupa habari hii kwa mfano wa hadithi kuwahusu ndugu wawili.

Majina ya hawa ndugu wawili yanatambulika kwetu mno – Kaini na Habili. Hadithi yaeleza kwamba Kaini alikuwa na wazo la kumtolea Mungu sadaka. Na kwa maana alikuwa mkulima wa ardhi, yeye aliyaleta mazao ya ardhi kama sadaka kwake Mungu. Naye ndugu yake alikuwa ni mchungaji wa kondeni, na hivyo basi yeye

aliitoa sadaka ya mnyama. Sadaka yake Habili ilikubalika lakini yake Kaini ilikataliwa.

Watu wengi hukosea kwa kudhania kwamba sadaka yake Habili ilikubalika kwa kuwa ilikuwa ni sadaka ya mnyama. Lakini kwa hakika, huu siyo ukweli uliomo katika maandiko. Sadaka ya Habili ilikubaliwa kwa kuwa yeye mwenyewe alikubalika kwake Mungu. Sadaka ya Kaini ilikataliwa kwa kuwa yeye binafsi hakukubaliwa naye Mungu.

Unapoijia hadithi yake Kaini na Habili, ni rahisi mno kusoma mambo ambayo hayamo ndani yake. Kaini hakuwa ameagizwa amlete mnyama kama sadaka. Kwa hakika, katika kitabu cha Walawi, watu walikuwa wameagizwa kuleta nafaka au mazao ya mbegu. Mimea kama hii ndiyo ilidhaminiwa zaidi. Hivyo basi, namna ya sadaka haikuwa na umuhimu katika hadithi hii; ni watu wenyewe ndio walikuwa muhimu. Kaini alikuwa hajakubalika, na alipogundua hili yeye alishikwa na hasira na kuvunjika moyo.

Kama jinsi ile alivyowatendea wazazi wake Kaini, Mungu anauliza swali: “Mbona umekasirika? Na mbona uso wako umekujamana?”(Msitari 6) kwa hakika Mungu anafahamu sababu yake vyema zaidi. Lakini ugumu wa moyo wake Kaini haupokei ujumbe, na kwa hivyo basi Mungu anaendelea: “kama ukitenda vyema uso wako utainuliwa? Na kama usipotenda vyema, dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe na ni sharti uishinde” (Msitari 7). Jambo la kuvunja moyo ni kwamba, Kaini anashindwa kuishinda dhambi yake. Katika msitari 8, twaelezwa kwamba yeye alimuua ndugu yake.

Na kwa mara nyingi swali laja: “Ndugu yako yuko wapi? Umetenda jambo lipi?” walakini Kaini, angali na moyo mgumu, akataa kuikiri dhambi yake hadi wakati Mungu anapo dhihirisha kwamba yeye tayari afahamu yale yaliyotendeka (Tizama msitari 9-10).

Mwanzo 3, swali lilikuwa, “Wewe upo wapi?” na Mwanzo 4, swali lilikuwa, “Ndugu yako yupo wapi?” Mungu alipoliuliza swali hili, alikuwa akijaribu kumfanya Kaini atambue yale yaliyokuwa tayari yametokea – kwamba alikuwa amemtupia hasira yake mtu asiyekuwa na hatia, na kwa hakika, bado alikuwa nayo hasira.

Matendo yake hayakuwa yametatua lo lote lile; badala yake, yalikuwa yameharibu mambo zaidi.

Tukirudi nyuma kidogo, msitari 7 ndio ufunguo wa hadithi hii yote. Unakabiliana na kiina kikuu cha kutofautiana, na kutoa suluhisho: kama ukiyatenda yaliyo mema, utakubalika kwake Mungu, utajikubali mwenyewe, na hautatembea katika maisha huku ukingombana na watu wengine.

Watu wengi hufikiri kwamba kifungu hiki chatueleza kuwa tusiwahukumu watu wengine. Ukweli ni kwambaYesu alikuwa akisema yale ambayo Mungu alikuwa akijaribu kumweleza Kaini: “Unatizama jambo bovu. Wacha kufadhaishwa naye ndugu yako, bali jitazame wewe mwenyewe.”

La furaha ni kwamba, kifo chake Habili hakikuwa kifo cha wema. Baada ya vizazi viwili, katika Mwanzo 4:26, tunaona kwa mara ya kwanza mwanadamu akianzisha mawasiliano na Mungu, au maombi. Hadi hapa, mawasiliano yote yalianzishwa na Mungu.

Sote hukabiliana na pingamizi nyakati zote. Mara nyingine sisi ndio huwa chanzo cha kutofautiana huku. Wakati mwingine siyo sisi. Lakini wakati wo wote ule ambapo unakumbana na pingamizi, jaribu kutawala hisia yako hadi utakapojiuliza mwenyewe kiini cha shida yako ni kipi. Kisha ufanye jinsi kifungu cha Mwanzo 4:7 kinavyokueleza wewe. Yaani kutenda yaliyo mema.

Sura ya 9
Baba wa Imani

Tumefikia sehemu iliyo kubwa katika kitabu hiki cha Mwanzo. Sehemu hii yahusu na watu watatu wanaofahamika vema katika Bibilia: Ibrahimu, Yakobo, na Yusufu. Kumbuka kwamba kiwango kinacho pewa sehemu fulani hutueleza na kudhihirisha umuhimu wake. Somo kuu katika sehemu hii ya Mwanzo ni imani. Huku tutakapo kuwa tukizisoma sura zifuatazo, Mungu atutaka kufahamu imani kama ilivyokuwa na ilivyo wakati huu.

Wahebrania 11, ambayo pia inajulikana kama sura ya Imani, ina haya ya kusema kuhusu swala hili:

> “Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.” (Msitari 6)

Kwa maana Imani ni ya muhimu na Mungu atutaka sisi kufahamu kuhusu imani, Yeye atueleza hadithi ya mtu aitwae Ibrahimu. Mtu huyu yutajwa zaidi ya mtu ye yote yule katika Agano Jipya. Iwapo unataka kuelewa imani, wahitaji kumwelewa Ibrahimu.

Jina Lake

Mtu huyu ni mfano mzuri wa imani. Tunapokutana naye kwa mara ya kwanza mwishoni mwa kitabu cha mwanzo sura ya 11, jina lake ni Abramu, linalo maanisha “Baba wa wana wengi.” Jina la mzaha kwa mtu wa miaka 75 asiye na mwana hata mmoja! Hata hivyo Mungu alimwambia Abramu kwamba yeye “angaliufanya uzao wake kama vumbi ya ardhi; ili kama yupo mtu awezaye kuhusebu vumbi aweza kuwahesabu pia.” (13:16). Tunapoangalia jinsi Abrahamu alivyotii Mungu kwa uaminifu, twaweza kutambua kwamba Abramu alimuamini Mungu kwa swala hili la uzao. (tizama Mwanzo 16.)

Madhabahu Yake

Wakati mwingi sisi hudhani kuwa wito ni kujiunga na kundi au shirika fulani. Lakini hatudhani kwamba Mungu anaweza kutuita kwake tu. Hebu fikiria ingalikuwa iwapo Mungu angekuita na akuongoze kwenda jangwani kuu isiyo na watu na bila ya kukupa sababu? Haya ndiyo yale yaliyomtokea Ibrahimu akiwa mzee wa miaka 75 (Tizama 12:1-4).

Zipo pande mbili katika hadithi hii; upande wake Mungu, na upande wake mwanadamu. Ili kuona upande wake Mungu, tusome kuhusu kujidhihirisha kwake Ibrahimu. Mungu alijidhihirisha kwake Ibrahimu mara nane. Ni yeye aliyeuanza uhusiano huo, na huu ni ukweli katika kila uhusiano wake Mungu. Katika Warumi 3:11, Paulo atueleza kwamba hamna mtu amtafutaye Mungu. Ni Mungu anayemtafuta Mwanadamu. Kama mwanadamu akimtafuta Mungu,

yeye huwa akiuitika mwito wake Mungu aliyemtafuta. Mungu ndiye huuanzisha uhusiano kila mara.

Upande wake mwanadamu wa uhusiano, au itiko lake Ibrahimu kwake Mungu, huja katika mfano wa madhabahu manne ambayo Ibrahimu aliyojenga. Madhabahu ya kwanza yaliundwa katika nchi tambarare ya More, pale Mungu alipomtokea na kumwambia, “Kwa vizazi vyako nitawapa hii nchi” (12:7). Neno hili More lamaanisha “Kufundisha au kutafuta.” Madhabahu haya ya kwanza twayataja kama kuwa “Madhabahu ya itiko” kwa kuwa yalijengwa kwa kuitikia mwito wake Mungu aliyekuwa akimwongoza katika nyikani.

Dhabahu yake ya pili yaliundwa kati ya Hai na Betheli. Katika Kihebrania, Betheli humaanisha “Nyumba ya bwana.” Na kwa kuwa Mungu hakuwa nayo nyumba wakati huu, neno hili laonekana kumaanisha “Mahala ambapo Mungu yupo.” “Warumi 6:23 yasema Mshahara wa dhambi ni mauti,” na miji hii yawakilisha haya. Kwa upande mwingine wa mashariki mbali na Hai upo mji wa Sodoma na Gomora. Katika madhabahu ya kwanza, Ibrahimu alikuwa akisema, “Nifundishe mimi.” Katika madhabahu haya ya pili,kulingana na jinsi yilivyoandikwa, yaonekana kuwa hakuwa ameamua jinsi atakavyo kubali kile Mungu alikuwa akimfunza.

Baada ya tukio hili, Ibrahimu alirudi katika mahala pale pa madhabahu yake ya pili na kumuitia Mungu. Baada ya majadiliano walisikizana naye Lutu kutengana. Maandiko hayatuelezi yale waliyoyazungumza, lakini yaonekana kwamba Mungu alikuwa amezungumza naye na kumwonyesha kwamba hakustahili kumchukua Lutu alipokuwa akisafiri kuenda pale alimoishi. Na jinsi tunavyo ona Lutu akitumbukia dhambini huko Sodoma na Gomora twaweza kuelewa ni kwanini.

Lutu alisafiri kwenda mashariki; Ibrahimu akasafiri kwenda upande wa magharibi. Hapa aliyaunda madhabahu yake ya tatu mahala palipojulikana kama Hebroni. Neno Hebroni lamaanisha “Ushirika.” Neno hili ni la mfano pia. Ambapo madhabahu ya kwanza yalisema, “Nifundishe mimi,” na madhabahu ya pili yalisema, “mimi sina uhakika,” madhabahu haya yaonyesha, “Mungu, nataka kukufahamu mimi.” Madhabahu haya tutayaita “madhabahu ya ushirika.”

Katika sura mbili za kwanza kuhusu hadithi ya Ibrahimu, yaani sura ya 12 na 13, aliyaunda madhabahu matatu. Hakujengi madhabahu mengine hadi katika sura ya 22. Ni yapi yale yaliyotendeka katikati ya madhabahu ya tatu na yale ya nne?

Wakati Ibrahimu aliposema, “Mungu, nataka kukufahamu wewe,” nafikiri Mungu alimjibu “Ibrahimu, kama wataka kuwa na uhuisano na mimi, ningalipenda ufahamu kitu fulani. Kama mimi ni kitu, mimi ni mambo yote. Kwa sababu kabla unione mimi kama mambo yote, basi hujaniona kama kitu.” Nayo maisha yake Ibrahimu yalikuwa na mambo mengi ambayo yeye hakutaka kuyaachilia.

Katika Mwanzo 16, tunamuona Ibrahimu na Sara wakiwa na hofu ya jinsi Mungu angalitimiza ahadi kuhusu uzao wake – na kwa sababu hiyo waweza kumsaidia Mungu. Kwa mawaidha yake mkewe, Ibrahimu akahusika naye mjakazi wake Sara, Hajiri. (Msitari 1-4). Mtoto aliyezaliwa katika uhusiano huo alikuwa ni Ishmaeli, ambaye ndiye baba yao Waarabu. Siku ya leo hakungalikuwa kashfa ye yote iliyoko Mashariki ya Kati kama Ibrahimu hangefanya alivyofanya.

Naamini kwamba Sara anawakilisha shida ya namna nyingine katika uhusiano wake Ibrahimu na Mungu. Madhabahu ya tatu, Madhabahu ya Uhusiano, yahusika na uhusiano uelekeao juu na ule uelekeao upande. Hautenganishwi. Ili kumfahamu Mungu, inambidi Mungu kuchukua nafasi yake katika maisha yake Ibrahimu. Ilimbidi Mungu kuzungumza naye Ibrahimu kuhusu Lutu na kumtoa Lutu toka maishani mwa Ibrahimu. Ilimbidi pia kumtoa Ishmaeli maishani mwake Ibrahimu. Baadaye alimtokea Ibrahimu na kuuambia amfukuze Ishameli. Mmoja baada ya mwingine. Mungu anawaondoa hawa watu ambao wanaichukua nafasi ya kwanza katika maisha yake Ibrahimu.

Sara ni shida sampuli tofauti. Sara ni mfano wa watu ambao Mungu huwaleta katika maisha yetu ila hatuwatambui kama kuwa ni Mungu aliyewaleta kwetu. Ilimbidi Mungu kumtokea Ibrahimu mara mbili kumhusu Sara. Mara ya pili, akasema, “Kumhusu Sarai mke wako, hautamwita Sarai tena bali Sara ndilo litakalo kuwa jina lake. Nami nitambariki, hakika nitakupa mwana kumpita yeye.” (17:15-16).

Mwaka mmoja baadaye, mwana wa kiume alizaliwa kwao Ibrahimu na Sara, naye Mungu akawaambia wamwite Isaka, ambayo

maana yake ni “Kicheko.” Mungu hakutaka hawa mashujaa wa imani kusahau kwamba wao walimchekelea wakati Mungu alipo waambia yale angeyatenda.

Mwishowe, wakati Isaka alipofanyinka kijana, Ibrahimu aliunda madhabahu mengine, na haya ndiyo yalikuwa ya muhimu zaidi. Yalijengwa kwenye mlima wa Moria. Moria maana yake ni “Yehova atatoa.” Hadi wakati huu Ibrahimu ndiye alikuwa akichagua mahala pa kuyajenga madhabahu, lakini haya madhabahu ya nne ni ya tofauti. Kwa mara hii, Mungu ndiye anachagua pa kuyajenga. Wakati huu pia, Mungu anachagua sadaka ya kutolewa – Isaka.

Mbali na kuwa mtoto wa kipekee katika siku za uzee wa Ibrahimu na Isaka, yeye ndiye akayetimiza imani yao ya miaka ishirini na mitano ya imani. Kisha Mungu anasema kitu cha ajabu hapa. “Namtaka Yeye.” Naye Ibrahimu anamchukua yule kijana hadi juu ya mlima huku akitetemeka, ilhali anakusudia kutenda yale ambayo Mungu alikuwa akimwambia atende. Lakini katika dakika ya mwisho, alinapodhibitisha utiifu wake, Mungu anampa Ibrahimu mwana kondoo badala ya uhai wake Isaka (Tizama 20:1-19).

Ujumbe wa Bibilia waweza kujumlishwa kwa maneno mawili, “Mungu Kwanza.” Siyo rahisi, lakini pia hamna ugumu wo wote ule. Aitha yeye ni Mfalme maishani mwako, au sio. Kwake Ibrahimu alikuwa ndiye Mfalme.

Sura ya 10
Wewe U Nani?

Hadithi ya Yakobo ni ya kusisimua mno. Katika hadithi yake Yakobo, baada ya kumdanganya baba yake na kuunyakua urithi wake na baraka, mama yake alimjia na kumshauri, “Ni lazima uondoke, Yakobo, Kwa kuwa ndugu yako atakuua wewe. Nenda ukaishi na ndugu yangu Labani kwa siku chache hadi hasira yake ipungue” (Tizama 27:42-43).

Usiku wa kwanza Yusufu alipokuwa akisafiri, alipata ndoto. Katika ndoto hii aliona ngazi ambayo malaika walikuwa wakishuka chini na kupanda juu. Katika ndoto hii, Mungu alimtokea na kumdhibitishia Agano aliyomfanyia Ibrahimu, Babu yake Yakobo.

Mungu alimwaahidi Yakobo kwamba yeye pia atakuwa sehemu ya mpango, huku akiongezea kwa kusema, “Mimi ni pamoja nawe, na nitakulinda popote utakapokwenda, na kukurudisha katika nchi hii; sitakuacha hadi nitakapoyatimiza yale niliyokuahidia wewe” (28:15).

Yakobo aliamka katika ndoto yake huku amejawa na mshangao mkuu. “Kwa hakika Mungu alikuwepo mahala hapa, nami sikufahamu,” akasema (Msitari 16). Na kabla ya kuendelea na safari yake, alichukua jiwe alililolitumia kuegemeza kichwa chake kama mto(pillow) na kumwagilia mafuta, huku akitoa nadhiri kwamba atamtolea Mungu fungu la kumi toka kwa yote yale atakayompa (Misitari 18-22).

Vita yake Yakobo

Yale yanayo fanyika hapo baadaye ndiyo sehemu kuu katika hadithi.

> “Yakobo akakaa peke yake; na mtu mmoja, akashindana naye mweleka hata alfajiri. Naye alipoona ya kuwa hamshindi, alimgusa panapo vungu wa paja lake; ukateguka uvungu wa paja la Yakobo alipokuwa akishindana naye. Akasema, Niache, niende, maana kunapambuzuka. Akasema, Sikuachi, usiponibariki. Akamwuliza, Jina lako ni nani? Akasema, Kwa nini waniuliza jina langu? Akambariki huko. Yakobo akapaita mahali pale, Penueli, maana alisema, Nimeonana na Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imeokoka.” (32: 24-30).

Tizama swali ambalo Mungu amuuliza Yakobo: “Jina lako ni nani?” Katika nyakati za Bibilia, majina yalikuwa ni ya muhimu mno, kama tulivyo gundua tayari. Yalieleza kumhusu mtu na pia yalimtambulisha mtu. Na kwa swali hili, hakika Mungu alikuwa akimuuliza Yakobo jina lake. Alikuwa akimwuliza, “Wewe U nani?” na siyo kwamba alitaka kulifahamu jina lake, ila kwamba alitaka Yakobo kufahamu jibu lake. Jina Yakobo, kama tunavyo fahamu, la maanisha “Mnyakuaji.” Lakini jina lake Israeli, jina ambalo uzao wake wote utaitwa la maanisha “Mpiganaji.”

Lipo jambo lingine lenye umuhimu mno katika hadithi hii ambalo twahitaji kulitambua. “Baraka ya Taji kwa kuvunjika,” na

kwa sababu Yakobo alikuwa ni mtundu mno, ilimbidi Mungu kumvunja ili ambariki.

Wakati mwingine Mungu hawezi kutukaribia kwa njia nyingine ye yote ile, na kwa sababu hiyo lazima atuvunje sisi kwa njia fulani, ili kutulazimisha sisi kumtegemea yeye. Haya ndiyo yaliyomtokea Yakobo. Na mwishowe, Yakobo akaupata ujumbe. Alipokutana naye Esau mwishowe – ambaye, kwa hahika hakupigana naye, bali alimwangukia shingoni na kumbusu yeye – akamwambia ndugu yake kwamba yeye alikuwa nao hawa wake wote na watoto na mifugo kwa kuwa "Mungu ameninemeesha mimi." (33:11). Na siyo kwa sababu alimnyakua yeye, bali kwa sababu ya neema yake Mungu.

Mungu pia hutufundisha kunyenyekea kwake. Wakati mwingi yeye huchagua kutuvunja kwanza, ili kwamba atubariki. Kwa hakika twahitajika kutizama sehemu tatu ili tutambue twahitajika kuwa nani. Kwanza, twahitaji ***kutizama juu***. Katika masomo yote tutakayo yasoma tutambue kwamba wakati mwingi humchukua Mungu kuwafanya watu ***kutizama juu***. Lakini kumtizama Mungu ni lazima tujifahamu sisi ni nani na twahitajika kuwa nani. Ukweli ni kwamba ni Mungu aliyetuumba. Anayo ramani ya maisha yetu mikononi mwake.

Lifuatalo ni kwamba, twahitajika ***kutizama ndani***. Katika Zaburi 139, Daudi aliomba, "Nichunguze mimi, ee Mungu, na uufahamu moyo wangu, nijaribu na uyafahamu mawazo yangu. Chunguza kama umo uovu wowote ndani yangu, na kuniongoza mimi katika njia ya milele" (Msitari 23-24). Sote twahitaji kumuuliza Mungu kututizama sisi ndani ya mioyo yetu na kutuonyesha sisi tu nani na sehemu ambazo hazitakikani.

La kumalizia, twahitajika ***Kutizama kote kote***. Mtu yule ambaye ametizama juu na kwa hakika ametizama ndani yu tayari kutizama ***kote kote*** na kuhusika na watu wengine na kufanyika sehemu ya mpango wake Mungu kwa ulimwengu.

Ushawahi kutizama juu kwake Mungu na kuyaona yale anayoyasema kuhusu kitambulisho cha utu wako ndani yake? Ni mara ngapi unatizama juu na kuichunguza hali ya moyo wako? Je! Watizama kote kote ili kuyaona yale Mungu anayokutakia katika kuhusika nao watu wengine katika maisha yako?

Sura ya 11
Mungu aliye kwenye Usukani

Tumesoma kuhusu Ibrahimu, ambaye alimefunza kuhusu Imani. Tumemtizama Yakobo, aliyetuonyesha neema yake Mungu. Sasa twamjia Yusufu, ambaye hadithi yake yazijaza sura 14 za mwisho katika Kitabu cha Mwanzo.

Yusufu atambulikana kuwa mojawapo wa watu walio kuwa bila lawama katika maandiko. Kwao watu wengi Mungu hutuonyesha unyonge wao pamoja na uwezo wao, lakini Yusufu ni wa kipekee katika haya (Mwingine ni Danieli, ambaye tutamtizama hapo baadaye katika masomo yetu).

Hadith yake Yusufu

Hadithi yake Yusufu kwa hakika yahusu rehema yake Mungu. Ujumbe wa hadithi hii wajumlishwa na msitari mmoja katika Agano jipya Warumi 8:28, usenaosema, “Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.” Ndugu zake Yusufu waliona aibu walipomgundua yeye ni nani, lakini akawageukia na maneno haya ya faraja – maneno ya kuwadhibitishia kwamba Mungu huhusika nayo mambo yote katika maisha yetu pia:

“Basi sasa, msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku; maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu . . . Kuwahifadhia masazo katika nchi, kuwaokoa ninyi kwa wokovu mkuu. Basi si ninyi mlionipeleka huku, ila Mungu. (Mwanzo 45: 5, 7-8).”

Katika hadithi ya Yakobo, baba yake Yusufu, tuliyaona maisha yake yakiwa mazuri - si kwa ajili ya bidii yake- ila ni Mungu aliyekuwa usukani wa maisha haya. Ijapo kuwa hadithi ya Yusufu inayo tofauti, inaangazia hoja hii hii. Katika hadithi yake, twayaona maisha yake mtu ambayo kwa wakati fulani hayakuonekana yakienda vyema. Aliuzwa katika utumwa, na kushitakiwa bila hatia ye yote ile. Alisahauliwa na wale waliomuahidi kumsaidia yeye. Matukio haya yote haya kuwa katika kutoka kwa matendo yake. Alikuwa akipitia

hali ngumu na mbovu; siyo kwa sababu alipaswa kupitia hali hizo, ila kwamba Mungu apate kutukuzwa na mipango yake kutimilika.

Tunayopaswa Kujifunza

Hadithi inayo mambo kadha tunayopaswa kujifunza na kuyatenda katika maisha yetu. Kwanza, hebu tizama uhusiano wake Yusufu na baba yake pamoja na ndugu zake. Uhusiona wao haukuwa wenye mfano wakutamanika! Yakobo hakuwa mfano mwema wa mzazi. Upendeleo wake kwa Yusufu ulimletea Yusufu shida nyingi kuliko raha – hii haikuwa haki kwao nduguze.
Lakini ni nani miongoni mwetu aliye nao wazazi wakamilifu? Ni wangapi miongoni mwetu wenye uhusiano mwema na ndugu zetu? Hatukuzichagua jamii zetu, ingawaje watu wa jamaa zetu hutupa mwongozo wa maisha yetu. Wengi wetu tuna majeraha, kuvunjika moyo na majonzi kwa ajili ya uhusiano huu wa kijamii. Hivyo basi ujumbe wake Yusufu kwetu sisi ni huu: Mungu ni mweza yote na ndiye yupo usukani katika maisha na hali zote maishani mwetu. Hamna hali ye yote iliyo mbovu ambayo hawezi kuikomboa na kuwa na wema. Mungu aweza kuwatumia ndugu na dada zako hata kama wao wana unyonge katika maisha yao. Mungu anaweza kukutumia wewe kwa jinsi unavyo husika nao katika kuyaongoza maisha yako. Siku moja utatambua jinsi walivyo husika katika kukutayarisha ili uitenda kazi ambayo Mungu amekupangia wewe.

Sura ya 12
Mwanzo wafikia Ukingoni, na Kutoka kwaanza

Tunapojifunza Bibilia, na hasa mno kuchunguza Agano la Kale, twahitaji kutambua maendeleo ya ujenzi wao hawa watu makhususi. Katika kitabu cha Mwanzo twasoma kwamba hawa watu walizaliwa kumpitia Ibrahimu. Yakobo naye akawapa jina, Israeli, naye Yusufu aliwaokoa kutoka maafa ya njaa. Wakati kitabu cha Mwanzo kinamalizika, taifa hili lilikuwa la jamii kumi na mbili peke yake, na jamii hizo zilikuwapo Misri.

Kitabu cha Kutoka kinapoanza, kundi hili lao watu ambao hawakuwa wamefanyika kuwa taifa walikuwa wameongezeka kuwa kundi kubwa. Kabla yao kufanyika kuwa taifa, wao walimhitaji kiongozi. Kitabu cha Kutoka kita tueleza kuhusu moja wa viongozi wakuu katika historia yao watu wake Mungu, Musa.

Shida moja kuu ambayo Musa alikumbana nayo katika kuliongoza kundi kubwa hili la watumwa ilikuwa kwamba hao hawakuwa nayo sheria, wala mwongozo. Hakuwa nayo taratibu ya uongozi kwa watu hawa. Na hivyo katika kitabu hiki, tutaona baadhi ya sheria ambazo Mungu alimpa mwanadamu, Amri Kumi.

Musa alikuwa na shida nyingine: alikuwa na watu wa kweli ingawaje walikuwa mahali ambako hawakustahili kuwepo. Walikuwa katika utumwa na Mungu aliwahitaji wawe huru. Neno **Kutoka** yaani **(Exodus)** lamaanisha, “njia ya kutoka nje.” Na sehemu kubwa ya kitabu hiki yazungumzia kuwahusu wana wa Israeli wakiipata njia ya kutoka nje kutoka utumwani.

Kitabu cha kutoka, zaidi ya kuwa ni historia, pia ni hadithi ya mfano. Hakika wana wa Israeli walikuwa ni watumwa huko Misri; Hata sisi bila Kristo, tumo katika utumwa wa dhambi zetu. Kitabu cha Kutoka cha husika nayo shida ya kuwatoa watu wa Israeli kutoka katika utumwa wao wa kimwili; Bibilia yote yahusika na shida ya kuwatoa watu chini ya utumwa wa kiroho.

Je! Ushawahi kuwekwa huru kutoka chini ya utumwa wa dhambi ambao Mungu ameutoa kwako? Katika sura ifuatayo tutaendelea kukisoma kitabu cha Kutoka. Anza kukisoma sasa, huku ukijiuliza hayo maswali matatu ya muhimu: Yasema nini? Yamaanisha nini? Naweza kuitimiza namna gani katika maisha yangu?”

Sura ya 13
Kumfanya Mtu Yeye Asiye Mtu

Ili kukielewa kitabu cha Kutoka, wahitajika kuwaelewa **Watu, Shida** na **Nabii**. Kitabu cha Kutoka ni hadithi yao watu wake Mungu na jinsi walivyotoroka utumwa chini ya uongozi wa Musa.

Jumbe Kuu Tatu

Neno kutoka lamaanisha “Njia ya kutoka nje.” Ujumbe wa kitabu cha Kutoka ni huu kwa hakika: njia ya kutoka nje ya utumwa huu ni ipi? Utumwa huu, kwanza ni wa kimwili, na hadithi kuhusu ukombozi kutoka katika utumwa huu ni mojawapo ya muujiza mkuu katika Bibilia. Ni hadithi ya kweli na ni Historia. Jinsi haya yalivyo tokea na yale yaliyo husika ndio ujumbe wa kusisimua katika kitabu cha Kutoka, na huu ndio mtizamo wa kwanza katika kitabu hiki.

Mbali na kuwa kitabu cha kutenda na cha historia, kitabu hiki kinao ukweli ulio katika hadithi ya mfano mzuri iwezayo kutumika katika maisha yetu ya ibada. Yale tunayojifunza ni haya: Sisi pia tu watumwa. Hatuwezi kuyatenda yale ambayo tungetamani kutenda ila tunatenda yale tunayolazimika kutenda. Hivyo basi ikiwa tunatenda mambo yale tuna lazimika kutenda, wala si yale tungetamani kutenda, basi sisi tu watumwa. Na kama sisi hatupo huru, sisi tu watumwa na twahitaji suluhisho. Twahitaji kuutafuta ukombozi wetu kutoka kwa utumwa wa dhambi. Neno wokovu, ambalo sote twalifahamu, lina maana sawa na neno ukombozi, hasa katika Agano la kale. Wokovu ni ukombozi tokana na dhambi. Na si adhabu ya dhambi sasa na siku zijazo pekee, bali pia nguvu za dhambi.

Jambo la tatu ambalo twa hitajika kutilia mkazo katika kitabu cha Kutoka ni Nabii Musa. Ukiwalinganisha watu wengine wake Mungu katika maandiko Musa ndiye kinara. Kwa hakika Musa ndiye mmoja wa watu wakuu waliowahi kuishi. Waweza kuuona ukuu wake Musa unapofahamu kazi aliyomfanyia Mungu. Ibrahimu ndiye aliyewazaa watu wake Mungu na kama tulivyosema hapo mbeleniYakobo ndiye aliwapa jina, Yusufu naye akawaokoa. Lakini Musa, aliyoyatenda twaweza kuyatizama katika kitabu cha kutoka.

Changio La Musa

Kwanza, Musa ndiye aliyewapa hawa watumwa uhuru. Wengi wetu hatufahamu maana yake kuwa watumwa. Watu wanapokuwa kifungoni jambo kuu linalowasumbua ni tamani ya kufanyika huru. Musa alipowapa uhuru, aliwapa watumwa kitu kubwa walichokuwa

wakitaka. Kisha Musa akawapa watu hawa waliokuwa huru kwa sasa kitu kingine walichohitaji- Serekali, au Sheria.

Katika ulimwengu wa kiroho, Musa aliwapa watu hawa wake Mungu mambo mawili yenye dhamani kuu. Aliwapa wao Neno lake Mungu, na pia akawapa ibada.

Wakati watu wanapoisoma Bibilia, wao hufanya vyema katika kukisoma kitabu cha Mwanzo na kujifunza kuwahusu watu waliomo ndani yake. Halafu yapo matukio makuu katika kitabu cha Kutoka, ukombozi kutoka Misri ambao huwapa shauku ya kuendelea zaidi. Walakini wanapofikia robo tatu ya kitabu cha Kutoka na kuingia katika kitabu cha Walawi, wao hujiona kama wamekwama kusonga mbele. Unaposoma sehemu hii, waiona ni kama sehemu ya mwongozo. Na hivi ndivyo ilivyo. Wakati unapofahamu kitabu hiki cha mwongozo sababu yake ni nini, utaanza kusisimuka. Huu ni mwongozo wa ibada.

Tukiachwa peke yetu sisi hatufahamu jinsi ya kuabudu. Jinsi wanafunzi wake Kristo walivyomuuliza Yesu awafundishe kuomba, nao wana wa Israeli walihitaji kufunzwa jinsi ya kuabudu. Nasi pia twahitaji kufunzwa. Katika makanisa ambayo huwa na taratibu za ibada, mhuduma wa kanisa huelekeza mgongo wake kwao watu wake huku uso wake ukitizama miimbari wakati mwingi. Haya makanisa pamoja na Sinagogi katika imani ya kiyahudi yana kina chake cha kuabudu kutoka katika hema la ibada ambalo Mungu alimwongoza Musa kulijenga.

Ningalipenda kuyatazama maisha yake Musa kwa mwelekeo huu. Shida kuu iliyomo katika kitabu hiki cha Kutoka ni shida ile ya utumwa. Suluhisho lake ni ukombozi, na Mungu alimwita Musa kuwa ndiye mkombozi. Kama jinsi kitabu cha Kutoka ni mfano wa ukombozi, maisha yake Musa ni mfano mmoja mkuu wa jinsi ya mkombozi.

Hadithi yake Musa

Kukombolewa kutoka katika mamlaka ya dhambi, ndio ujuzi mkuu unaoweza kuwa nao katika maisha. Jambo lingine kuu ni kufanyika chombo kinachowawezesha wengine kukombolewa.

Waweza kuyatizama maisha yake Musa katika nyakati tatu, kila moja ikiwa miaka 40. Katika miaka 40 ya kwanza somo kuu ambalo Mungu amfundisha Musa ni, Musa, wewe si kitu."

Na kwa kupitia mazingara ambayo hayakuwa ya kawaida, Musa alilelewa katika jumba la kifalme lake Farao (Tizama kutoka 1-2:10). Na labda kwa sababu hii yeye alijifikiria kuwa ni mtu bora zaidi yao wengine. Lakini wakati huu alikuwa na umri wa miaka arobaini, Mungu alifaulu kumshawishi kwamba yeye alikuwa ni mtu duni. (Tzama 2:11-15).

Somo la pili ambalo Mungu alimfunza Musa lilitukia katika miaka arobaini ya pili ya maisha yake. Wakati huu, ujumbe ulikuwa, "Musa, wewe ni kitu kwa kuwa ni mimi niliyekuchagua wewe." Mwisho mwa mika ya arobaini ya pili, Musa alikwenda kutembea nje na akawaona Waebrania walivyo kuwa wakiteseka kama watumwa, huku akifahamu kwamba hata yeye alikuwa ni mtumwa wa kiebrania. Na katika sura ya 2:11 twasoma,

> "Hata siku zile, Musa alipokuwa mtu mzima, akatoka kuwaendea ndugu zake, akatazama mizigo yao. Akamwona Mmisri anampiga Mwebrania, mmojawapo wa ndugu zake."

Na wazo ambalo kifungu hiki kinatufundisha ni kwamba aliwaonea huruma, na alihusika kabisa katika hali yao na katika kuteseka kwao.

Na muda tu baadaye, Musa alikuwa huko jangawani na akaona kichaka kikiwaka moto bila ya kuchomeka. Hili halikuwa jambo kubwa sana mahala pale. Kwa kawaida vichaka viliteketea katika sekunde tano. Lakini wakati huu, haikuwa hivyo. Kichaka hakikuteketea; kiliendelea kuwaka moto bila ya kuteketea. Musa akaenda kujionea kile kilichokuwa kikitokea (3:1-3). Tizama yale yanayotukia baadaye:

> "Bwana alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame, Mungu akamwita kutoka katikati ya kile kijiti, akasema, Musa! Musa! Akasema, Mimi hapa. Naye akasema, Usikaribie hapa; vua viatu vyako miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. Tena akasema, Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo.

Musa akaficha uso wake; kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu.” (Kutoka 3:4-6).

Hebu fikiria kuhusu kushtuka kwake Musa! Kwa ufupi, masomo haya mawili – kwamba Musa alikuwa si kitu, na kwamba Musa alikuwa kitu wakati Mungu alipokuwa naye – yakiunganishwa yanaonyesha unyenyekevu. Mungu alimchagua Musa kwa kuwa alifahamu kwamba Musa amejifunza kumruhusu Mungu kufanya kazi kupitia yeye.

Watu wengi waliomo katika mamlaka hufanya bidii ili kuwachagua watu ambao wamefaulu ili kufanya kazi za muhimu. Katika Bibilia, yaonekana kwamba Mungu hujaribu kuwachagua watu ambao hawajahitimu kulingana na kipimo cha binadamu. Na kama tutatumiwa naye Mungu katika kuwakomboa watu siku ya leo, kama tukihitaji kuwaona baadhi yao marafiki wetu au wapendwa wetu wakikombolewa kutoka kwa utumwa wa dhambi, twahitaji kukumbuka hili: Siyo sisi ambao twawakomboa wao.

Somo Kwetu Sisi

Mtu mnyenyekevu hufahamu ni nani anayeitenda kazi. Mtu huyu husema, “Ni mpango wa Mungu kutumia uwezo wake katika watu wake ili kukamilisha makusudi yake kulingana na mpango wake Mungu.”

Katika kitabu cha Kutoka, Mungu ni kama Mzabibu, naye anatafuta matawi ili kuwa sehemu ya mzabibu. Mungu hawezi kutenda kazi bila ya chombo. Kwa sababu hiyo, ni lazima Mungu ampate Musa wake. Hapo anapo mchagua Musa wake, ni lazima amshawishi. Lazima amwabie, “Musa, wewe si kitu. Si wewe utakayeyatenda haya. “Unapoyafahamu haya Musa, basi wewe unakuwa mtu ambaye naweza kumtumia, naweza kutenda kazi ndani yako na waweza kugundua muujiza mkuu wa jinsi ninavyoweza kumtumia mtu aliyetambua kwamba yeye si kitu.”

Sura ya 14
Pingamizi Za Kibinadamu na Siri Za Kiroho

Tumeona jinsi Mungu alivyo mtayarisha Musa kwa kazi yake ya kuwakomboa wana wa Israeli. Siku ya leo tutatizama siri zake Mungu ambazo alishiriki naye ili kumpa mafanikio; na tutaona jinsi Musa alivyo uitikia mwito wake Mungu.

Siri zake Mungu za mafanikio zaweza kujumlishwa kwa maneno haya: "Kumbuka kwamba wewe siwe mkombozi – Mimi ndimi. Wewe binafsi huwezi kumkomboa mtu ye yote. Mimi naweza, na nipo pamoja nawe. Lakini lazima yawe ni mawazo yangu na siyo yako wewe." Siri hizi zilikuwa za kweli kwake Musa, na ni za kweli kwetu sisi pia. Alimfudisha Musa haya katika kichaka kilicho kuwa kikiwaka.

Musa alihangaishwa na sababu yake yakutoweza kujieleza vyema. Hii yamaanisha kwamba labda alijifikiri kuwa yeye hakuwa ni mnenaji hodari, au labda kwamba alikuwa na udhaifu wa kuzumgumza. Labda alikuwa nacho kigugumizi au kusitasita. Cho chote kile, yaonekana kwamba Mungu alikifahamu na alimtaka yeye ingawaje alikuwa na unyonge wake. Na kwa hakika Mungu alimtaka yeye kwa sababu ya hali ya unyonge wake. Waweza kuona kwamba Mungu alitaka ukombozi huu utakapotendeka, uwe ni kwa sababu ya nguvu zake mwenyewe na wala si kwa sababu ya umaarifa wake mtu ye yote yule. Na hii ndiyo sababu alimtaka Mwebrania, mchungaji wa Kondeni, na labda mtu aliyekuwa nacho kigugumizi, ili kwenda mbele ya uso wake Farao huku akidai kuwachiliwa huru kwa watu wake. Watu wake walipowekwa huru, Mungu hakumtaka mtu ye yote yule kusema, "hayo yalitendwa na Musa. Yeye alikuwa mnenaji bora. Nilikuwepo hapo wakati alipoudai uhuru wa watu wake. Ilikuwa ni jambo la kusisimua mno!" Mungu hakutaka iwe namna ile. Na ndio sababu alimchagua yule mtu aliyemtaka. Tizama maneno yaliyomo katika msitari wa 11:

> "Bwana akamwabia, Ni nani aliyekifanya kinywa cha mwanadamu? Au ni nani afanyaye mtu kuwa bubu au kiziwi, au mwenye kuona, au kipofu? Si mimi, Bwana?"

Maswali haya ni magumu mno kwa watu wengine kuyachukua. Yaonekana kuwa yale Mungu anayoyasema kwa mara nyingine ni lile somo tulililoliona katika maisha yake Yusufu: hali ya maisha yako huundwa na Mungu mwenyewe. Labda hautafahamu sababu yake, lakini Mungu hutufanya sisi kuwa jinsi tulivyo. Naye Mungu alikuwa akisema haya kwake Musa, “kama nilimtaka mtu mnenaji, ningalikufanya wewe kuwa mnenaji?

Kufikia mahala hapa, Mungu alimpatia somo la mfano. Mungu alimuuliza hivi, “Ni kitu gani ulicho nacho katika mkono wako?” Naye Musa akasema, “Fimbo ya mchungaji.” Naye Mungu akasema, “itupe fimbo hiyo chini.” Wakati Musa alipoitupa ile fimbo chini, ilibadilika na kuwa kitu ambacho Mungu amekitumia sana katika huduma yake Musa, nyoka. Halafu Mungu akaendelea kumwambia aweke mkono wake ndani ya koti lake na kuutoa tena nje. Alipoutoa nje, ulikuwa na ukoma. Mungu alimwambia kurudia hilo tendo nao mkono wake ukapona (Msitari 2-7).

Mungu alikuwa mvumilivu mno kuhusu pingamizi zake Musa. Lakini wakati anapomwambia Mungu, “Tafadhali mtume mtu mwingine,” (Msitari. 13), ilimfanya Mungu kupandwa hasira kinyume chake. Sasa twashangaa, wakati Mungu anapokupa mwito wa kuwa mkobozi, Je! Waweza kutoa pingamizi kama zake Musa? Je! Waweza kusema hivi: “Mtume mtu mwingine badala yangu mimi”? Watu wengi katika maandiko walikuwa ni watu wa kweli na wenye ujasiri wa kumwambia Mungu kwamba, “Mungu, mimi sitaki.” Haya ndiyo yale ambayo Musa alikuwa akiyasema. Na kwa maneno mengine, jambo hili ni jema, kwa kuwa yule atakaye kwa wakati mwingi ni wa kushukiwa.

Baada ya hayo yote, Musa alikwenda. Naye alifanikiwa. Hata hivyo fanaka haikuwa yake, bali ilikuwa ni ya Mungu.

Watu wengi wanao uwezo mwingi lakini hawana wakati wa kujitolea. Noa Wengine hawana uwezo ilhali wana nafasi ya kujitolea. Maandiko yasema kwamba haijalishi kama wewe unao uwezo mdogo au mwingi. Jambo lililo la muhimu ni katika kujitolea. Katika kazi yake Mungu, uwezo ulio mkuu ni ule wa kujitolea. Yeye hatutumii kuambatana na hali yetu ila yuatututmia bila kuangalia hitilafu zetu.

Mojawapo ya kweli muhimu ambazo Mungu alimfudisha Musa yaweza kujumulishwa kwa shairi hili fupi:

Mimi sipo, bali yeye yupo.
Mimi siwezi, bali yeye aweza.
Mimi sitaki, ila yeye ataka.
Mimi sikufanya, bali yeye alitenda.

Hizi ni Siri nne za kiroho.

Ni matumaini yangu kwaba waweza kujifundisha siri hizi nne za kiroho, kama Musa alivyo jifunza.

Sura ya 15
Janga, Miujiza, na Kanuni za Ukombozi

Sasa nigelipenda tutizame hadithi ya ukombozi ambayo picha yake imo katika kitabu cha Kutoka. Kama tulivyosema hapo awali, neno ukombozi ni sawa na neno Wokovu. Tutakapofika kitabu cha Kutoka katika somo la ukombozi kuhusu ujuzi wa wokovu walioupata hawa watu wake Mungu, sisi twauona uwezo wake Mungu. Hii ni kwa sababu hamna jambo kama wokovu wa wakati uliopita au wa wakati huu, bila ya uwezo wake Mungu. Katika kitabu cha kutoka, utauona uwezo wake Mungu ukidhihirishwa kwa njia ya kipekee kuanzia janga kumi.

Janga

Ujumbe wa janga kumi ni mfano wa kweli ambao unafundishwa katika Bibilia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Katika 1 Yohana 4:4, kweli hiyo yadhihirishwa kwa njia hii: “Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu.” Haya ndiyo mafunzo yatakikanayo kutendwa.katika ujumbe huu wa mapigo kumi.

Katika Kutoka 5:1, Musa na Haruni wamwendea Farao kwa dai lao la kwanza ili kuwaweka huru wana wa Israeli kwenda. Lakini Farao anawadhihaki tu. Kwa hakika haya yalionekana kana kwamba

ni mzaha tu. Musa hakumpa sababu hasa ambayo ilimshawishi awaache huru wana wa Israeli. Maelezo waliompatia Farao haya kuwa nayo maana ye yote ile: “Mungu wao Wahebrania alikutana nasi; na kwa sababu hiyo, turuhusu sisi twende kwa kuwa haya ndiyo ambayo Mungu ametueleza sisi kukueleza wewe. (Msitari 1).

Katika hadithi hii, twaona kitu ambacho sisi twaweza kukiita “Kanuni za ukombozi” kutokana na nguvu za dhambi au uovu. Musa anavyozidi kuamuru Farao awaachilie wana wake Mungu naye Farao anapozidi kukataa kuwaachilia, ndivyo mapigo yanavyoendelea. Nazo Janga zile, zina ushawishi wa kutosha. Kidogo kidogo, Farao anaanza kukiri nguvu zake Mungu. Huku akizidi kujitolea, hebu tizama mazungumzo kati yake Musa na Farao. Watu wengi huamini kwamba Musa ni mfano wa Mkombozi, Yesu Kristo, na kwamba Farao ni Picha yake Shetani, ambaye ndiye mfano kamili wa uovu. Kama tutayaelewa yale yanayoendelea kati yake Musa na Farao, twaweza kuyalewa yale yanayoendelea siku ya leo kati yake Yesu Kristo na Shetani.

Kwa mfano, yatazame yale ambayo Farao anayasema katika Kutoka 8:25 baada yake Musa kumtaka awaachilie wana wa Israeli ili kwamba waende kumtolea Mungu wao sadaka. “Mwaweza kumtolea Mungu sadaka, hata huku katika nchi ya Misri! Msiondoke katika nchi ya Misri!”

Mwishowe Farao akubali kuwaruhusu wao kuifanya sherehe yao ya kidini, lakini anatilia mkazo masikizano fulani: “Naam, mwaweza kuenda, ila musisafiri mbali” (Msitari. 28).

Hii pia ni picha ya njinsi mwamini anavyo songwa na kujaribiwa.

Sheatani yuamwambia “Ni sawa ikiwa wewe wataka kuwa mtu wa kidini. Walakini natumai kwamba wewe hutapata kuwa mshupavu kidini kiwango kwamba upoteze akili, au kutilia mkazo imani yako.”

Katika 10:8-10, baada ya janga zaidi, Farao aanza kukubali kidogo. “Naam mwaweza kuenda, lakini hamtasafiri pamoja nao watoto wenu. Mtawaacha Misri.” Wakati shetani anapogundua kwamba hawezi kuilegeza imani yetu, yeye hujaribu katika kuwapata watoto wetu. Ni jambo la kushangaza jinsi watu wengi wameipokea

imani wao wenyewe, huku wakiwaacha watoto wao Misri. Hii ni hila yake Shetani ambayo yaonekana katika Farao.

Kanuni ya kwanza ya ukombozi ni kwa kujitenga na dhambi. Lakini kama tayari upo katika dhambi kama watu wengine, mtu hutorokea wapi? Kitabu cha Kutoka cha tueleza: Ili kutoka katika utumwa na utawala wa kimabavu wa dhambi wahitaji muujiza. Twaiona picha ya mfano wa miujiza ambao twauhitaji ili kuvuka bahari ya Shamu. Muujiza huu uliwakilisha sehemu ya mwisho ya ukombozi kutoka kwake Farao. Katika majadiliano yote kati ya Musa na Farao, waweza kufahamu kwamba siyo nia yake Farao kuwaachilia wana wa Israeli wawe huru. Farao azidi kubadilisha badilisha mawazo yake. Anaposema "Nendeni," yeye yuabadili jibu lake mara tu mapigo ya janga yanapopungua na kusema "hamuwezi kuenda." Hata kuwapa uhuru, Farao anaubadilisha moyo wake. Wakati watu wake Mungu wanapo fika ukingo wa Bahari ya Shamu, anawakusanya wanajeshi wake, na yaonekana kwamba Farao atawaangamiza wote.

Miujiza

Musa anayatenda yale Mungu anamwambia atende. Twaifahamu hadithi yote vyema. Maji yaligawanyika kama kuta mbili, nao wana wa Israeli wakavuka katika nchi kavu. Farao alipojaribu kuwafuata wana wa Israeli, kuta hizo zalitoweka na maji yakayaangamiza majeshi ya nchi ya Misri. (14:21-28).

Unapokaribia miujiza ya Agano la Kale, yakubidi kuamua kama wewe waamini miujiza au hauamini mambo yasiyo ya kawaida. Mimi nauamini huu muujiza. Naiamini ahadi hii jinsi ilivyo andikwa. Naamini kwamba ilitendeka kama ilivyo andikwa. Hakika hadithi hii ni mfano wa wokovu wetu sisi. Huchukua muujiza ili kukuokoa wewe. Humchukua Mungu muujiza ili kutokomboa sisi, na muujiza huu wa Bahari ya shamu ni picha yetu sisi.

Wakati wana wa Israeli walipoichukua hatua ili kupita katika Bahari ya shamu na kuvuka hadi jangwani, kulitokea shida mpya, iliyokuwa kuu. Je! Hawa watu wangekula na kunywa nini katikati ya utupu mkuu wa jangwa lile? Halaiki ya watu zaidi ya Milioni mbili

au tatu walihitaji chakula na maji. Musa hakuwa na wazo lo lote lile kuhusu la kutenda. Lakini Mungu alifahamu.

Mungu anawatendea muujiza kwa kuwalisha hawa watu wote kimuujiza. Asubuhi moja walipoamka, kulikuwa na kitu cheupa kilicho tandazwa chini kote. Wakauliza, “Ni nini hii?” Tafsiri ya “ni nini” kwa lugha ya Kiebrania ni “Mana,” na hili ndilo jina ambalo walikiita chakula hiki. Tangu wakati ule, kilitokea kila asubuhi na kila jioni. Pia Mungu aliwatumia ndege waitwao Pare nao wakakuwa chakula chao pia.

Chakula ambacho Mungu aliwapa wana wa Israeli kilikutana na mahitaji yao yote ya kimwili. Nao wakaishi wakila chakula hiki kwa miaka arobaini. Huu ni muujiza mwingine wa Mungu ambao twahitaji – yaani kutuhifadhi. Je! Ni nani anaye kutana na mahitaji yako? Wategemea uchumi wa nchi au wajitegemea wewe mwenyewe kukutana na mahitaji yako? Kiini hasa cha vitu ambavyo twahitaji ni Mungu. Tunapomtizama Yeye, atakutana na mahitaji yetu. Tunapomshukuru Mungu kwa chakula kabla ya kukila, tunakiri kwamba yeye ndiye mwenye kutupa chakula kile na pia ndiye anayetupa vyote tunavyohitaji. Matoshelezo yake Mungu kwao wana wa Israeli wakati wa miaka arobaini waliyo tangatanga nyikani yatukumbusha kuhusu ukweli wa utoshelezaji wake Mungu.

Ukombozi wetu

Katika kitabu cha Kutoka, twagundua misingi ya taratibu muhimu zaidi wakati wa kuabudu. Sacramenti iliyopo katika kina cha ukombozi wao wana wa Israeli imefanyika kuwa ni sacramenti iliyo katika kiini cha wokovu. Janga la mwisho ambalo Mungu alilimwaga Misri liliwahusisha wazaliwa wa kwanza katika kila nyumba ya Wamisri. Kwa upande mwingine watu wake Mungu walikuwa wameamuriwa kutoa dhabihu ya kondoo na kunyunyiza damu yake milangoni mwa nyumba zao. Siku ya leo tumehifadhiwa kutoka mauti ya milele kwa sababu ya Yesu Kristo, mwana kondoo wake Mungu, aliyetolewa dhabihu kwa ajili yetu. Damu yake ndiyo inayo tuokoa. Yesu Kristo ndiye kondoo wa Mungu anayefanaishwa na kondoo aliyechinjwa siku ya wana waisraeli kutoka utumwani na ndiye yeye ambaye kifo chake kilichukua dhambi za ulimwengu.

Maombi yangu ni kwamba unapokisoma kitabu cha Kutoka, utaweza kuona miujiza iliyotendeka ili kuwaokoa wana wa Israeli na tutambue kwamba miujiza hii hii hutuokoa sisi.

Sura Ya 16
Roho Ya Amri Kumi

Ningalipenda sasa tusonge kwenye Amri Kumi, kama zilivyonakiliwa katika kitabu cha Kutoka 20:1-17. Kwa maana amri hizi kumi zafunika amri zingine nyingi zaidi, tunapozitazama hizi kumi tutakuwa tumezitazama zote zile nyingine.

Amri Kumi ziliandikwa katika vibao viwili vya mawe. Katika kibao kimoja kulikuwemo Amri Nne, zote zile ambazo zina mwongozo wa uhusiano kati yetu na Mungu:

1. Usiwe na miungu mingine ila Mimi.
2. Usijifanyie sanamu ya kuchonga,
   wala mfano wa kitu chochote kilicho
   juu mbinguni, wala kilicho chini duniani.
3. Usilitaje bure jina la Bwana
4. Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.

Amri hizi nne zahusika nao uhusiano wetu na Mungu.

Kibao cha pili kilikuwa nazo Amri sita juu yake, nazo Amri hizo sita zahusika na uhusiano wetu nao watu wengine.

1. Waheshimu baba yako na mama yako
2. Usiue.
3. Usizini
4. Usiibe
5. Usimshuhudie jirani yako uongo
6. Usimshuhudie jirani yako uongo.

Hebu tuzitazame sheria kwa undani zaidi zaidi ili tuone maana yake kamili.

Sheria ya kwanza yasema, “Usiwe na miungu mingine Ila Mimi.” Yasemekana kwamba Bibilia yaweza kujumlishwa katika

maneno mawili: “Mungu Kwanza.” Nahili ndilo jambo lililo katika sheria ya kwanza.

Sheria ya pili hutukataza sisi kuiunda sanamu ye yote ile yenye mfano wa cho chote kile kilichoko mbinguni au duniani na kukiita Mungu. Sheria hii hutukataza kuwa waabudu wa sanamu. Kwa maneno mengine, kiini cha sheria hii ni: Mungu ni Roho. Twahitajika kumwendea Mungu kwa imani.

Kwa jinsi Mungu ni Roho, kiini cha imani yetu hakitaonekana wakati wowote ule. Hivi ndivyo Mungu hutaka. Yeye hututaka tumwendee kwa imani. Kama tukikiunda kitu kutokana na vitu vionekanavyo na kusema kwamba hivyo vitu vyamuwakilisha Mungu, tunatupilia mbali haja ya imani.

Sheria ya tatu ilikuwa kwamba tusilitaje jina lake Mungu bure. Ingawaje watu wengine hudhani kwamba hili lamaanisha kulitaja wakati wa kutoa maneno ya matusi tu, asili ya sheria hii ni kuu zaidi. Yamaanisha hivi: Wakati wo wote unapolitaja jina lake Mungu, hata katika ibada, ni vyema ukikumbuka hivi kuwa hustahili kumtaja ovyo ovyo bila ya kufikiria au kwa dharau.

Sheria ya nne yasema tuikumbuke siku ya Sabato na kuifanya kuwa takatifu. Neno hili lilikuwa nayo maana na matumizi mengi. Sheria nyingi za Wayahudi zilitokana na sheria hii, ila hii kanuni yafanana na ile sheria ya kwanza: Mfanye Mungu kuwa wa kwanza. Tenga wakati kwa ajili yake. Matumizi mengine ya kanuni hii ya Sabato ni kupumzika kwa kawaida.

Unapoutazama ubao wa pili utakuta sheria zinazowahusu watu katika maisha yako. Ya kwanza ni dhahiri, kwamba yahusika na wazazi wako. Katika maisha yako ya kawaida, hawa ndio watu utakaohusika nao kwanza. Hii ndiyo sheria iliyo na ahadi; kama ukiwaheshimu baba na mama yako, siku zako zitakuwa nyingi katika ulimwengu (Msitari. 12). Hebu tizama hiyo amri. Yamaanisha kuwa “heshimu” na wala siyo “kuwatii” wao. Bibilia pia husema kwamba watoto wawatii wazazi wao. Wakati wewe ni mtoto watakikana kutii. Lakini sheria hii yawazungumzia watu wazima pia, nayo yatuambia kuwaheshimu baba na mama. Na sababu moja kwa nini hili ni la muhimu, ni kwa sababu yawaonyesha watoto wako jinsi wastahili kukutendea wewe.

Sheria ifuatayo yasema usiue. Haisemi kwamba usiuwe kwa kuwa zipo sehemu ambazo Mungu amewaamuru watu wake kuwauwa watu wengine (Tizama Mwanzo 9 na Warumi 13, baadhi ya nyingine). Maana ya amri hii ni kwamba uhai upo katika mikono yake Mungu; na Mungu ndiye huutoa uhai na hivyo jukumu lake kuuchukua uhai huo.

Sheria ya saba yatuambia sisi tusizini. Naamini kwamba roho ya sheria hii ni ile ambayo ya maanisha "haki zao watoto." Ni mpango wake Mungu kama ilivyotajwa hapo katika Mwanzo 2, kuwachukua watu na kuwafanya washirika, ili kwamba wafanyike kuwa wazazi na kuwazaa watu ambao watafanyika kuwa ni wazazi na washiriki. Ndoa ndipo mahala penye usalama ambapo Mungu angalipenda watoto kulelewa na kutayarishwa katika maisha. Usalama wao watoto, hivyo basi, hutegemea usafi katika watu wawili waliooana. Haki ndilo jambo kuu katika sheria hii. Hii ndio sababu Mungu asema, "Usizini."

Sheria ya nane ni, "Usiibe.' Roho ya sheria hii ni kuwa Mungu ni Mungu wa taratibu. Kutegemea neema yake pamoja na upanzi na uvunaji wetu, sisi hukusanya rasilmali zingine katika maisha yetu. Unapoiba, waitupilia mbali taratibu ambayo Mungu aliyokusudia.

Sheria ifuatayo ni, "Usimshuhudie jirani yako uongo.' Hii ni moja wapo ya sheria ambayo watu wengi hawajaitazama kwa uangalifu. Sisi hufikiria kuhusu uongo mkubwa na uongo mdogo. Njia moja ya kushuhudia uongo ni kuwa kusema ukweli nusu. Watu wengi ni hodari katika tabia hii hasa wakati ambapo wataka kuwadhulumu watu wengine. Ila Bibilia yasema: "Usimshudie jirani yako uongo." Haijalishi werevu unaotumia. Kama nia yako ni kusema ukweli nusu, au kutoitaja kweli, wewe tayari umeivunja hiyo sheria. Kiini cha sheria hii ya tisa ni kusema ukweli mtupu.

Sheria ya mwisho yasema, tusitamani. Kiini cha sheria hii yafanana na ile ya nane, "usiibe." Mungu ana nia kuhusu yale tuliyo nayo. Mke tulie naye, nyumba tuliyo nayo, cheo tulicho nacho na kwa jumla sehemu tulipo maishani. Mungu ana wajibu katika mambo hayo yote. Maandiko yanatuanuru dhidi ya kujilinganisha na watu wengine. Kila mmoja wetu ni wa kipekee. Wakati Mungu alituumba mimi na wewe, aliitupilia ramani mbali. Hakutaka sisi tufanane. Na kama jambo hili ni la kweli, hatustahili kujilinganisha na watu

wengine. Wivu na tamaa hudhihirisha kutotosheka kwetu na mapenzi yake Mungu maishani mwetu.

Sura ya 17
Hema la Ibada

Watu wengi wanapoisoma Bibilia hukiona kitabu cha Walawi kuwa kitabu kigumu mno. Wao hukiona ni kitabu cha kuchosha unapokisoma hasa taratibu na michoro ya hema la ibada.

Neno walawi la maanisha, “Kuambatana na jamii ya Lawi.” Walawi, kwa hakika walikuwa ni makuhani wa kiyahudi. Ili kukielewa kitabu cha walawi, ni vyema kama wafahamu kuhusu hema lililofahamika kama “Hema lililokuwa nyikani”. Kisha baadaye likaitwa Hekalu la Sulemani na lilikuwa na umaridadi usio na kifani. Lilijengwa kulingana na ramani ile ya kwanza ya Hema ya ibada ambayo Musa alipewa ramani yake ili kuijenga.

Kitu kikubwa kuhusu Hema La Ibada kilikuwa kwamba hema hili lilikuwa katikati ya kambi. Ukweli kwamba Hema ya ibada lilikuwa katikati lina mfano fulani. Sheria ya kwanza ilisema kuwa Bwana yuastahili kuwa kwanza katika maisha ya watu wake. Maandiko yatufunza kwamba Mungu atakikana kuwa katikati ya maisha yetu yote. Hili laonekana kwa jinsi kwamba Hema la ibada lilijengwa katikati ya kambi ile.

Labda jambo lililo la muhimu mno ambalo twaweza kuliona kutoka katika Hema la Ibada ni kwamba Mungu kwa hakika aliishi katika hema lile dogo. Tunaelezwa wakati Mungu alipomaliza kulijenga hema la ibada, uwepo na utukufu wake Mungu uliijaza ile hema, kuonyesha jinsi Roho Mtakatifu anavyoyajaza maisha yao waamini siku ya leo.

Huku wana Waisraeli wakisafiri nyikani, wingu lililo ning’inia juu ya hema liliwaongoza. Wingu liliposonga, wao walilifuata. Wakati liliposimama, wao walisimama. Wingu liliwaongoza wao. Watu walilikaribia hema wakitafuta msamaha, wakiabudu na kutafuta mwongozo.

Jinsi Ya Ujenzi wa Hema

Kwa kuwa sasa twaifahamu sababu ya hema, hebu tutazame kwa undani ujenzi wake. Hema hili la ibada lilikuwa na ua- wa kamba iliyofanana na hema- uliozunguka pande zote. Eneo la ndani mwa ua lile palikuwa na uwanjamdogo. Hapo baadaye uwanja huu ungepanuliwa zaidi wakati wa Suleimanii. Uwanja huu kwa wakati ule haukuwa mkubwa katika Hema ya Ibada ya kwanza.

Kulikuwa na vyombo fulani katika Hema la Ibada ambavyo vilikuwa ni vya muhimu mno. Ni vyema kama tukitambua kwamba kila chombo katika Hema ya Ibada kilikuwa na kishikio chake. Hili lilikuwa ni jambo la muhimu kwa kuwa vilibidi kubebwa wakati wote huko nyikani.

Chombo cha kwanza kiliitwa Madhabahu ya Shaba, ambacho kiliwekwa kwenye uwanja. Moto uliwaka wakati wote katika madhabahu haya ya Shaba. Wakati mwenye dhambi alipokuja hemani kutafuta msamaha, angelikutana naye kuhani katika lango la uwanja ule.

Kisha, mnyama wa kutolewa sadaka angechinjwa kulingana na maagizo katika Walawi. Baadaye, mnyama angewekelewa juu ya madhabau haya ya Shaba na kuhani. Naye mwenye dhambi angebakia katika lango la uani. Hangeliweza kuingia katika Hema la Ibada. Kuhani ndiye aliyeingia humo ndani badala yake. Kwanza, kuhani aliwekelea mnyama katika madhabahu yale ya shaba. Huku moshi wa sadaka ukipanda juu kumwelekea Mungu. Kuhani naye alienda kwenye chombo kingine kilicho itwa Birika. Hapa ndipo kuhani alijitakasa kwa niaba ya mwenye dhambi, aliyebakia malangoni ya uwanja.

Ndani mwa hema kulikuwa kumegawanywa sehemu mbili. Sehemu ya nje ilijulikana kama *Patakatifu* na *Patakatifu pa Patakatifu*. Kulikuwa na pazia zito ambalo lilitenganisha kati ya Patakatifu na Patakatifu Pa Patakatifu. Hapa Patakatifu pa Patakatifu ndipo Mungu alipoishi. Pazia lilijengwa na nyuzi nzito. Josephus msomi wa kiyahudi asema kwamba farasi kadha kama wangalivuta pande zote za pazia ile, haingepasuka. Pazia iliokuwa katika hekalu lake Sulemani na ililokuwa katika hekalu wakati wake Kristo ni kama ile inayokuwa kwenye majumba ya sinema au michezo ya kuigiza.

Twaelezwa katika vitabu vya Injili kwamba Yesu alipoiaga dunia, Pazia ambalo lilikuwa kati ya Patatifu na Patakatifu Pa Patakatifu, lilipasuka kutoka juu hadi chini (Tizama Marko 15:58). Huu ni mojawawapo wa miujiza mikuu ya Bibilia ambao hutambuliki sana.

Vilikuwa vyombo vinne katika Hema Ya Ibada. Baada ya kujitakasa, kuhani alikwenda katika Patakatifu.

Upande wake wa kushoto kulikuwa na kinara cha mishumaa. Mishumaa hii ilikuwa yenye umuhimu. Ilionyesha mfano wa Ufunuo wake Mungu ambapo Mungu aliwapatia watu wake Neno la Mungu – na hivyo basi, ufunuo huu ulionyesha jinsi ya kumwendea Mungu. Hivyo basi kuhani angaliabudu karibu ya Mishumaa na kumshukuru Mungu kwa ufunuo wake ambao alimpa mwenye dhambi aliyekuwa nje.

Upande wake wa kulia, kulikuwa Meza ya Mkate wa wonyesho. Kusudi lake lilikuwa ni kuonyesha kile chakula cha Mana kilivyokuwa, na kwamba Mungu hutupa sisi mkate wa kila siku au riziki yetu.

Mbele yake, kulia na juu ya pazia ambalo lilizuia njia ya kwenda Patakatifu Pa Patakatifu, kulikuwa na madhababu ya Uvumba, kuhani angalisimama na kuyafanya maombezi kwa niaba ya mwenye dhambi ambaye alisimama nje, uwanjani. Kuhani angalifika mahala hapa halafu kurudi ili kukutana naye mwenye dhambi mwingine na kuifuata taratibu ile ile tena.

Watu walikusanyika na kuzunguka Hema Ya Ibada mara moja kwa mwaka. Katika tukio hili, Kuhani angalipita katika pazia hadi Patakatifu Pa Patakatifu, na kutoa sadaka ya damu kwa dhambi ya watu wote.

Huku tukitizama hema la Ibada, twahitaji kufahamu kwamba kila chombo kilicho kuwepo mle kilimwakilisha Yesu Kristo. Na hivyo basi, hebu tuvitazame kwa makini na ubinafasi zaidi.

Vyombo vya Hekalu

Madhababu ya Shaba huzungumza kuhusu Injili katika Agano Jipya. Wanyama wote waliotolewa sadaka katika Madhababu haya, sadaka zote zilitimizwa wakati Yesu aliposulubiwa juu ya msalaba.

Madhabahu haya ya Shaba ya maanisha, “Huwezi kumkaribia Mungu mtakatifu bila ya sadaka. ‘Bila ya kumwagika kwa damu hamna msamaha wa dhambi.’” Tizama Waebrania 24:4).

Chombo kinacho fahamika kama birika, ambapo kuhani alijitakasa kabla ya kuingia mahala patakatifu, la maanisha yale ambayo maandiko yanayoyasema sehemu nyingi: “Ni nani atakaye panda juu katika mlima wake Mungu? Ni yule mwenye mikono safi na moyo safi.” (Zaburi 24:4).

Ushirika na Mungu ndio kusidi kuu zaidi watu walipoingia kwenye hema la ibada. Mambo yote huegemea upande huo. Na Bibilia hufananisha ushirika kati ya mtu na Mungu na kula. Birika maana yake ni sawa na jinsi mama yetu alipokuwa akituambia tukiwa watoto, “Tuoshe mikono yetu kabla ya kukikaribia chakula mezani.” Jioshe kabla kuja mezani, kabla ya kushiriki na Mungu. Lazima uoshwe; lazima uwe safi. Huu ndio uliokuwa ujumbe wa birika.

Chombo kingine katika Hema ya Ibada, kilikuwa ni taa au kinara cha Mishumaa ya Dhahabu. Wakati kuhani aliposimama mbele ya taa hii ya dhahabu, alikuwa akikubali kwamba Mungu ndiye chanzo cha kitabu hiki tunachojifunza. Alikuwa akimuabudu na kumshukuru Mungu kwa kumpa mwenye dhambi aliye nje ufunuo wa jinsi angaliokolewa na kumkaribia kwa njia ya kumwabudu Mungu.

Lifuatalo, hebu tutazame Meza ya mkate wa Wonyesho. Katika meza hii kulikuwepo mkate, ambao uliwakilisha ukweli kwamba Mungu ndiye mdumishaji wao watu wake na hukutana na mahitaji yao. Ukweli ni kwamba Mungu hangelipenda tupoteze ufahamu kwamba yeye ndiye hutupa riziki yetu.

Hebu tutazame katika Madhababu ya uvumba. Huku kuhani akisimama mbele ya madhabahu, alimwombea mwenye dhambi ambaye alikuwa nje ya lango la uani. Huku akitenda hayo, alikuwa yeye ni mfano wake Yesu Kristo, Kuhani wetu Mkuu, ambaye hutuombea sisi mbele zake Baba.

Kila kitu katika Hema lile la Ibada kilizungumza kumhusu Yesu. Yeye ndiye nuru ya Ulimwengu. Yeye ndiye Mkate wa Uzima. Yeye ndiye sadaka Kamili. Yeye ndiye huja na kutusafisha katika birika. Kwa hakika ni injili yake Yesu Kristo tunayoiona katika Hema ya Ibada. Na ni wakati tu unapofahamu kuhusu Hema ya Ibada ndipo

waweza kukielewa kitabu cha Walawi kwa kuwa kitabu hiki cha Walawi ni mwongozo ambao kuhani alitumia wakati wa kuongoza ibada katika Hema ya Ibada. Je! Wamfahamu huyu Yesu ambaye anaonyeshwa katika hema?

Sura ya 18
Hema Siku Ya Leo

Katika kitabu cha mwanzo, twasoma kwamba wakati mwanadamu anapotenda dhambi, tukio kubwa na ovu zaidi ni talaka – kutenganishwa – kati yake mwanadamu na Mungu. Suluhisho la upatanisho tokana na alaka ndio msingi wa ujumbe ulio kwenye bibilia. Na hii ndio maana kuu ya hema huko nyikani.

Hivyo basi mbona hatutoi sadaka za wanyama siku ya leo? Ni kwa kuwa matakwa yake Mungu yamebadilika. Tutakapo kifikia kitabu cha Waebrania tutayazungumzia haya zaidi. Lakini kwa ufupi, Waebrania 9 yasema kwamba Hema Ya Ibada ilikuwa mfano wa hema ambayo tayari imo juu mbinguni. Hema hii ya Kimbinguni haikuundwa na vitu vinavyo onekana. Imeundwa na vitu visivyonekana, vyombo vya kiroho. Hema ambayo Mungu alimwambia Musa aiunde ilikuwa ya kuonekana, na yaweza kuguswa na kudhihirishwa humu ulimwenguni kutokana na iliyopo mbinguni inayotajwa katika Webrania 9.

Kumbuka, wakati Yesu alipokufa juu ya msalaba, pazia katika hekalu lake Sulemani lilipasuka sehemu mbili-toka juu hadi chini. Kumbuka kwamba mara moja kwa mwaka Kuhani Mkuu aliingia katika Patakatifu Pa patakatifu, na kupeleka damu iliyozifunika dhamba zao watu wote. Kwa njia ile ile, wakati Yesu alipo kufa Msalabani alifanyika Kuhani Mkuu na huko mbinguni alipitia taratibu hii katika hema ya kimbinguni. Kwenye Madhabahu ya Shaba hekaluni la kimbingu, alitoa kifo chake kama timizo la mwisho la sadaka zote za wanyama. Alikwenda kwenye Birika ya Kujitakasa na kufanya iwezekane kuupokea usafi wa kudumu.

Kumbuka kwamba kulingana na kitabu cha Waebrania, ni hema la mbinguni ambayo inaipa ile ya hapa duniani umuhimu wake.

Katika Agano la Kale, hema lilikuwa ni mfano wa nje tu. Kilikuwa ni kitu cha kuonekana, kinacho dhihirisha ukweli wa kiroho ambao ulikuwa ukitendeka mbele ya uwepo wake Mungu wakati Yesu alipokufa msalabani.

Kabla ya kifo chake Kristo, mwenye dhambi hangelimkaribia Mungu. Ni kuhani peke yake ambaye angalimkaribia Mungu na kumwombea. Lakini haya yote yalitupiliwa mbali baada ya kifo chake Yesu. Wakati Yesu alikufa juu ya msalaba, alituwezesha mimi na wewe kuenda moja kwa moja hadi kwenye uso wa Mungu.

Jambo lingine la Muhimu ni kwamba miili yetu sasa ndiyo hekalu lake Mungu. Siyo kwamba twaijali hekalu hii sisi pekee, bali Mungu anahusika nayo pia.

"Je wafahamu kwamba Roho wake Mungu anaishi ndani yenu? Ye yote yule atakayeinajisi hekalu yake, Mungu atamharibu, kwa kuwa hekalu yake ni takatifu na hivyo ndivyo ulivyo."

Hebu fikiria hili – Kwamba uwepo wake Mungu kwa hakika waishi ndani mwetu! Mtume Paulo alijaribu kueneza kweli hii huko Korintho ambapo wengi wao walikuwa najisi kwa uasherati. Aliwaambia hivi, "Miili yenu haikuundwa kwa ajili ya uasherati, bali kwa ajili yake Mungu. Je! Mwatambua kwamba miili yenu ni hekalu yake Mungu, naye Mungu aishi ndani yenu?" Katika Wakolosai 1:27, yeye atuambia hivi, "Mungu ametaka kuwajulisha hao jinsi siri hiyo ilivyo kuu na tukufu ambayo imeenea kwa watu wa mataifa, nayo ndiyo hii: Kristo yuko ndani yenu, na jambo hilo lamaanisha kwamba nyinyi mtaushiriki utukufu wa Mungu."

Kristo ndani yako ni muujiza. Ya maanisha kwamba uwepo wake Mungu unaishi ndani yenu; na kwamba unakila kitu unachohitaji ili kuishi jinsi ambavyo Mungu amekuita kuishi.

Hebu sasa tutizama picha hii ya kuvutia kuhusu Hema Ya Ibada katika maisha yetu. Nakusihi ufanye hivi. Unapoamka asubuhi na kuanza wakati wako wa kimya na Bwana, wakati wa kuabudu, wakati wa kuwa kwenye uwepo wa Bwana, kabla ya kutoka nje na kuishi maisha yako siku ile, jaribu kuifikiria njia ya kupitia Hekalu la Ibada. Jifikirie ukipita karibu na Madhabahu ya Shaba ukiambatana naye mnyama na waenda kumtoa sadaka yule mnyama na fananisha na kifo chake Yesu Kristo kwa ajili ya dhambi zako. Kama wewe hujamtumainia Kristo kwa ajili ya msamaha wa dhambi zako, fanya

hivyo sasa. Halafu mshukuru Mungu kwa msamaha wako msalabani wake Yesu, kwa kuwa yeye ndiye sadaka kamili.

Jifikirie ukielekea katika Birika Ya Kujisafisha, ambapo utasafisha mikono yako na miguu yako, mahala ambapo wahitaji kufanywa safi kila wakati. Je ! vipo vitu katika maisha yako ambavyo ni vichafu, na havimpendezi Mungu? Ungama mbele yake Mungu; na ugeuke kutoka kwazo na kufanywa safi. Halafu kwa njia ya mfano, nenda katika Mahala Patakatifu na kusimama mbele ya kinara cha Taa ya Dhahabu na kumshukuru Mungu kwa Ufunuo, na kwamba yeye alikutoa kwenye giza.

Halafu jifikirie ukisimama kando ya Meza ya wonyesho, na umshukuru Mungu kwa kukutana na mahitaji yako yote. Mtambue Yeye kama ndiye chanzo chako cha kila mkate na rasilmali uliyonayo, na kwa vyote ambavyo yeye hukutosheleza kwazo. Mtambue kama yeye ndiye aliyekutana na mahitaji hayo, na kwa moyo wa shukrani. Unapowazia kuhusu Madhabahu ya Uvumba, fikiria muujiza wa maombi. Na uchukue wakati kuomba kabla ya kuendelea.

Ukiendelea kufikiria juu ya Patakatifu Pa Patakatifu, hebu hili likupe changa moto kufahamu kwamba kipo kitu kama Uwepo wake Mungu. Kumbuka kwamba Roho wake Mungu yupo ndani yetu nasi tupo katika uwepo wake Mungu po pote pale tulipo.

Zipo njia nyingi za ibada kutokana na mifano ya Hema nyikani. Hili ndilo la muhimu. Inawezekana kwake mtu mwenye dhambi kumkaribia Mungu Mtakatifu na kuwa katika uwepo wake kupitia kwa njia mpya na iliyo hai ambayo ilifanywa kumpitia Yesu Kristo Bwana wetu.

Je! Wewe ushakaribia katika uwepo wake Mungu Mtakatifu? Yesu asema, “Mimi ndimi njia, na ukweli na uzima, mtu haji kwa baba yangu ila kwa njia yangu.” Twaiona hii picha ya kiroho katika Hema la ibada. Mungu ataka kukutana na wewe na kuyafanya maisha yako kuwa ni Hema Yake.

Sura ya 19
Maana ya Sadaka

Sasa kwa kuwa twatambua yaliyomo katika Hema ya Ibada, tu tayari kukisoma kitabu cha Walawi.

Kitabu hiki hasa ni cha mwongozo kwao Makuhani. Ni kijitabu chenye taratibu kuhusu kuwachinja wanyama, yale yakufanya na nyama za matumbo na kadhalika. Hili labda si la kutia moyo kama Zaburi 23 au 1 Wakorintho 13, tafadhali usijihisi kana kwamba hamna kweli za kiroho ndani mwake au mambo ya kutimizwa ya kiroho ambayo waweza kujinufaisha nayo. Kitabu hiki kina kweli za kupendeza mno ndani yake, tutajaribu kutambua sehemu zenye kweli hizi.

Sehemu Hizi

Ni vyema kama ukitambua kwamba kitabu hiki cha taratibu zao makuhani kimegawanya katika sehemu kadha. Sura za kwanza saba zatilia mkazo kuhusu sadaka. Zamweleza kuhani yale yote anayopaswa kuyatenda wakati wa kuitoa sadaka, na pia zaeleza maana ya hizi sadaka.

Katika sura ya nane hadi ile ya kumi mkazo upo juu yao watumishi, au makuhani wenyewe. Maongozi katika sehemu hii yaeleza matakwa ya kuwa kuhani na kanuni ambazo kuhani atakikana kuzifuata. Mambo ya kutimizwa ni mengi mno katika sehemu hii.

Kina cha kitabu hiki cha patikana katika sura ya 11 hadi ile ya 22. Sehemu hii twaweza kuiita “utakaso.” Hema la Ibada pamoja na makuhani ambao walisimamia walikuwa ni wawakilishi wake Mungu kwa ulimwengu wote kwamba watu waliochaguliwa na Mungu ni watu watakatifu kwa kuwa Mungu wao alikuwa ni mtakatifu. Mkazo katika sura hizi ni kwamba hawa watu walikuwa wamechaguliwa kuwa tofauti. Neno “takatifu” lamaanisha “kitu kilicho chake Mungu.” Watu hawa walikuwa mali yake Mungu.

Katika sura ya 23 hadi 25 twaweza kuitaja kama sehemu ya “Huduma.” Zipo siku nyingi takatifu katika imani ya kiyahudi, na utazipata zimenakiliwa katika vitabu vitano vya kwanza kwenye Bibilia. Kwa kuwa makuhani walikuwa ndio viongozi watenda kazi

katika siku takatifu pamoja na sherehe takatifu, walihitaji mwongozo kuhusu jinsi ya kuyaendesha mambo haya.

Unapofikia sehemu hii ya Walawi, jiulize: Ni jambo gani ambalo Mungu aliwataka makuhani kukumbuka wakati alipozianza siku takatifu kama siku kuu ya Pasaka? Kisha jiulize tena swali hili: Mbona Mungu aliwataka wao kuyakumbuka mambo haya?

Sura mbili za mwisho za kitabu cha Walawi, twazitaja kama "Kusalimu Amri."

Kitabu hiki cha Walawi, kitabu cha kumbu kumbu la Torati na kitabu cha Yoshua vyafanana mno kwa njia nyingi. Zote zamalizia kwa wito mkuu kwao watu wake Mungu kwamba wazitii sheria zake Mungu na kuwa watu takatifu ambao Mungu aliwaita. Walikuwa wamekombolewa na kuokolewa ili kwamba wawe watakatifu. Maonyo katika sura hizi za mwisho katika kitabu hiki yana uwezo mwingi. Musa alikuwa amesema kwamba alikuwa nayo shida kubwa katika usemi wake, au kwamba hangaliweza kunena vyema, lakini yaonekana kwamba alikuwa ni mnenaji mzuri mno.

Matimizo

Hebu tutizame baraka ambazo twaweza kuzipokea katika kitabu cha Walawi. Tutaanza na sehemu ya kwanza, "Sadaka." Sura saba za kwanza za kitabu hiki zimo na kweli kuhusu jinsi makuhani walivyopewa mwongozo katika kuzitoa sadaka kwake Mungu. Kwa mfano, wakati mwenye dhambi alikuja katika Hema Ya Ibada kuutafuta msamaha, alikustahili kupatwa na kuhani mlangoni. Kuhani angalimwongoza yeye katika kumweleza maana ya dhabihu ambayo angeitoa, na yale aliyotakikana kusema.

Ya ziada katika wajibu wao, makuhani walikuwa ni waalimu wa watu wake Mungu. Huku mwenye dhambi akiitoa dhabihu yake, kuhani alimwongoza katika kuwekelea mkono wake juu ya kichwa chake yule mnyama. Mwenye dhambi alipotenda vile, dhambi yake ilipitishwa hadi kwenye kichwa chake yule mnyama. Kifo ambacho yule mwenye dhambi angelikipata kwa sababu ya dhambi yake kilimpata yule mnyama badala yake. Huu ndio uliokuwa umuhimu wa dhabihu ile.

Ukiendelea kusoma kitabu hiki, utagundua kwamba kulikuwepo nyakati ambapo taifa zima lilitenda dhambi, ilikuwa lazima toba ya taifa zima kufanywa. Walipogundua yale waliyoyatenda, iliwabidi kumtoa ndama kama dhabihu ya dhambi. Iliwabidi kuileta katika Hema, ambapo viongozi wa taifa zima wangalimwekelea mikono yao halafu wamchinje yule ndama mbele zake Mungu. Wangaliifuata taratibu ile ile kama ya dhambi ya kawaida. Na kwa njia hii, makuhani walifanya upatanisho kwa niaba ya taifa zima. Je! Si hili ni jambo zuri sana kutendeka kwa taifa zima? Toba ya taifa kwa dhambi ya taifa? Hili ni tendo ambalo lashauriwa kutoka katika kitabu cha Walawi.

Hawa makuhani walikuwa ni watu waliokuwa wamepakwa mafuta; hivi ni kusema kwamba walikuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Kuonyesha mfano huu, damu ya dhabihu iliwekwa juu ya sikio pamoja na mikono na kidole kikubwa cha mguuni wa kulia wake kuhani. Hii ilimaanisha kwake kuhani kwamba, “We u mtu mtakatifu. Watakikana kuwaongoza watu kuwa watakatifu. Kila kitu unachokisikia, unacho kigusa, kila utakapotembelea wahitajika kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu.

Katika kitabu cha Walawi, utaupata mfano mzuri mno kuhusu yale tunayoyamaanisha wakati tunaposema kwamba Musa aliandika kumhusu Yesu wakati alipokuwa akiviandika vitabu vya Sheria. Katika Agano jipya, wakati Yesu alipomponya yule mwenye ukoma, wakati wote alimwambia mwenye ukoma aliyeponywa, “Nenda ukawaonyeshe makuhani.” Mbona alisema hivi? Kwa kuwa katika kitabu cha Walawi yapo maagizo hayo.

Katika sura za mwisho za kitabu cha Walawi twayapata mahubiri mema mno yake Musa. Mambo ya kutimizwa ni dhahiri kabisa katika sehemu hii.

Kwa mfano, yeye amkariri Mungu akisema, “Kama mkifuata masharti yangu na kuzishika amri zangu, nitawanyeshea mvua wakati ufaao, nchi ipate kuzaa mavuno kwa wingi, nayo miti ya mashambani matunda yake. Kupura nafaka kutaenedelea mpaka wakati wa kupanda mbegu. Mtakuwa na chakula tele na kuishi kwa usalama nchini yenu. Nitawapeeni amani nchini hata mweze kulala bila ya kuogopeshwa na cho chote. Mtawafukuza adui zenu na kuwaua kwa upanga. Watano wenu watawafukuza adui mia moja na mia moja

wenu watawafukuza adui elfu kumi. Adui zenu wataangamia mbele yenu kwa upanga. Nitatembea kati yenu na kuwa Mungu wenu nanyi mtakuwa watu wangu. (Walawi 26:3…..12).

Utagudua kwamba katika kitabu cha Walawi yapo mambo yaliyokatazwa, kama mwanamume kufanya usherati na mwanamume mwingine. Maoni yangu ni kwamba tendo hili la ulawiti au ushoga lakatazwa kwa sababu sherehe ya matokeo yake ni mabovu. Tendo hili halilingani na mpango wake Mungu katika hali ya kufanyika wazazi au watu ambao wawazaa wazazi wengine. Musa anaihukumu tabia hii kwa ukali mwingi. Katika kitabu cha Walawi, Musa pia awahukumu wachawi, wasoma viganja, wenye kutabiri kwa kusoma nyota na mambo mengine mengi. Sheria zake Musa zilitiliwa mkaza mno kwa kuwa watu wa Kiyahudi walitakikana kuwa watu watakatifu. Utakatifu ndiyo msingi wa kitabu cha Walawi.

Ni matumaini yangu kwamba utangulizi huu wa kitabu hiki cha Walawi utakufanya ukisoma kitabu hiki binafsi na utabarikiwa ukifanya hivyo. Kumbuka, kwamba kitabu cha Walawi ni mwongozo kwao makuhani kwa jinsi ya kupakwa mafuta, watu watakatifu ambao wangaliwafundisha watu wake Mungu jinsi ya kuwa watakatifu. “Iwe ni watakatifu, asema Bwana” – Huu ndio ujumbe wa kitabu hiki cha Walawi kwako na kwangu mimi.